بسم الله الرحمن الرحيم

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU
MWINGI WA REHMA MWENYE
KUREHEMU

ß‰ƒ Ì • ãƒ $ y J ¯R Î) ﴿
| = Ï d õ ‹ ã ‹ Ï 9 ª ! $ #
ãN à 6Z t ã
}@÷ d r & §ô _ Í h • 9 $ # Ÿ
Mø • t 7 ø 9 $ #
ö / ä . t • Î d g sÜ ã ƒ u r
﴾ # Z Ž • Î g ô Ü s?

(al-Ahzaab: 33).

Zimepokelewa hadithi nyingi sana katika vyanzo na maswadir za kisunni na kishia juu ya (Kuhusiana na) kuteremka kwa aya hii tukufu ikihusiana na watu watano As'habul-kisaa (a.s), na kuhusika kwa istilahi ya (Ahlul-baiti) na wao pekee, nao ni: Muhammad (s.a.w.w) na Ali, Fatima, Hasan na Husein (a.s), kwa mfano rejea vitabu vifuatavyo:

Musnad Ahmad (241 h): juzu 1 / 331, na juzu 4 / 107, juzu 6 / 292 na 304. Sahihi Muslim (261 h): juzu 7/ 130. Sunanut-tirmidhi (279 h): juzu 5/ 361 na vinginevyo.As-sunanul-kubraa cha Nasai (303 h): juzu 5 / 108 na 113.Adhuriyyatut-twahirah Annabawiyyah cha Duulabi (310 h): juzu 8 /.Al-mustadrak alaa swahihaini cha Bwana Al-haakim An-naisaburi (405 h): juzu 2 / 416, na juzu 3 / 133 na 146 na 147. Al-burhan cha Zarkashi (794 h): 197. Fat'hul-bari Sharhu swahihul-bukhari cha Ibnu Hajar Al-askalani (852 h): juzu 7 / 104. Usulul-kafi cha Kulaini (328 h): juzu 1 / 287. Al-imaamatu wat-tabswirah cha Ibnu Baabawaihi (329 h): 47, H 29. Daaimul-islaam cha Maghribi (363 h): 35 na 37. Al-khiswal cha Swaduuq (381 h): 403 na 550. Al-amali cha Tuusi (460 h): H 438 na 482 na 783 vile vile angalia tafsiri ya aya hii katika kitabu Jaamiul-bayan cha Twabari (310 h). Ahkaamul-qur'an cha Jaswaas (370 h). Asbabun-nuzuul cha Al-waahidi (468. Zaadul-masiir cha Ibnul-jawzi (597 h). Al-jaamiu liahkaamil-qur'an cha Qurtubi (671 h). Tafsiru ibnu kathiir (774 h). Tafsiruth-thaalabi (825 h). Ad-durrul-manthuur cha Suyuutwi (911 h). Fat'hul-qadiir cha Shaukani (1250 h). Tafsirul-ayyashi (320 h). Tafsiirul-qumi (329 H). Tafsiru Furati cha Al-kufi (352 h) chini ya aya ya Ulul-amri. Majmaul-bayan cha Twabrasi (560 h) na vyanzo vingine vingi.

UKWELI KAMA ULIVYO

قَالَ رَسُولُ اللهِ 3:

إِنِّي تَارِكٌ فِيكُمُ الثَّقَلَيْنِ: كِتَابَ اللهِ وَعِتْرَتِي أَهْلَ بَيْتِي، مَا إِنْ تَمَسَّكْتُمْ بِهِمَا لَنْ تَضِلُّوا بَعْدِي أَبَداً، وَإِنَّهُمَا لَنْ يَفْتَرِقَا حَتَّى يَرِدَا عَلَيَّ الْحَوْضَ.

Hakika mimi nimeacha miongoni mwenu vitu viwili vizito, Kitabu cha Mwenyezi Mungu na kizazi changu Watu wa Nyumbani kwangu (Ahlul-Bait wangu), vitu ambavyo ikiwa mtashikamana navyo hamtapotea kamwe baada yangu na kwa hakika vitu viwili hivyo havitatengana: kamwe hadi vitakapo ingia kwangu kwenye Hodhi.

Imepokelewa kwa mfumo ulio karibiana katika Sahihi Muslim, juzu 7, ukurasa 122, Sunanud-daarimi, juzu 2 ukurasa 432, Musnad Ahmad, juzu 3, ukurasa 14,17, 26,59,na katika juzu 4, ukuras 366, 371, na juzu 5, ukurasa 182, Mustadrakul-haakim, juzu 3, ukurasa 109, 148, 533, na vyanzo vinginevyo.(Inapatikana katika vitabu Sahihi na Masaaniid)

UKWELI KAMA ULIVYO

Mwandishi:

SHEKH JAAFAR AL-HADIY

Mtarjumi:

ABDULMAJID NASSIR

JUMUIYA YA KIMATAIFA YA AHLUL-BAIT (AS)

نام كتاب: الحقيقة كما هي
نويسنده: جعفر الهادي
مترجم: عبد الماجد
زبان ترجمه: سواحيلي

Jina la kitabu: Ukweli Kama Ulivyo
Maudhui: Itikadi
Mtunzi: Shekh Jaafar al-Hadiy
Muandaaji:Kituo cha Utamaduni, idara ya Tarjuma Jumuiya ya Kimataifa ya Ahlul-Bait (AS)
Mtarjumi:Ustadh Abdulmajid Nassir
Mhakiki:Baraza
Upitiaji wa mwisho:
Mchapishaji:Kituo cha Uchapishaji na Usambazaji cha Jumuiya ya Kimataifa ya Ahlul-Bait (AS)
Chapa ya: Kwanza
Chapa ya: Israa
Idadi ya copy: 3000
Tarehe ya Usambazaji: 2008
Haki ya Usambaji imehifadhiwa na Msambazaji
ISBN : 978-964-529-361-9
www.ahl-ul-bayt.org
info@ahl-ul-bayt.org

YALIYOMO

TAMKO LA JUMUIYA YA AHLUL-BAIT 9
HAJA YA KUSHIKIANA NA KUELEWANA.....12
MADHEHEBU YA JAAFARIYYAH IMAMIYYAH..17

TAMKO LA JUMUIYA YA AHLUL-BAIT

Hakika urithi wa Ahlul-Bait (AS) ambao umehifadhiwa na madrasa yao, na wafuasi wake kuuhifadhi usipotee, unaelezea na kuibainisha ile madrasa iliyokusanya maarifa mbali mbali na ya aina tofauti ya Kiislamu.

Kwa hakika madrasa hii imeweza kulea nafsi na nyoyo zenye uwezo na maandalizi ya kunufaika na elimu hii kutoka kwenye mto huu wenye maji safi yenye kutiririka, na kuupatia Umma wa Kiislamu maulama wakubwa wenye kufuata nyendo na njia ya watu wa Nyumba ya Utume (Ahlul-Bait ar-Risaalah). Wameweza kujibu kwa njia bora na ya kukinaisha kabisa maswali na shubha za madhehebu na mielekeo mbali mbali ya kifikra iliyomo ndani na nje ya Uislamu katika kipindi chote cha historia na karne zilizopita.

Kwa hakika Jumuiya ya Kimataifa ya Ahlul-Bait (AS) kutokana na majukumu yake iliyojitwisha mabegani, inatekeleza wajibu wa kutetea heshima na utukufu wa Uislamu na ukweli wake ambao umefunikwa na ukungu wa viongozi wa makundi, madhehebu na watu wenye mielekeo ya kuupinga Uislamu. Ili kufikia lengo hilo, imekuwa ikifuata njia ya Ahlul-Bait (AS) na wafuasi wa madrasa yao yenye uongofu ambayo wakati wote imekuwa ikijibu, bila kusita wala kuchoka, maswali na changamoto zinazotolewa mara kwa mara kutoka pande mbalimbali. Imejaribu wakati wote kuendelea kubaki katika njia ya mapambano na kwa kiwango kihitajikacho katika kila zama.

Hakika uzoefu na tajriba iliyohifadhiwa kwenye vitabu vya wanazuoni wa Madrasa ya Ahlul-Bait (AS) kuhusiana na maudhui hii ni wa kipekee, kwani ni uzoefu wenye njia na nembo ya kielimu inayohukumiwa na akili na dalili za wazi,

na unaojitenga na kujiepusha na matamanio binafsi na taasubi iliyo kemewa. Unawazungumzia na kuwahutubia maulama na wanafikra wenye ujuzi maalumu mazungumzo yenye kuipendeza na kuivutia akili na kukubaliwa na maumbile safi ya kila mtu.

Kwa hakika Jumuiya ya Kimataifa ya Ahlul-Bait (AS) imejaribu kuwapatia watafuta-ukweli marhala na hatua mpya ya uzoefu huu ulio tajiri kupitia mijadala ya kielimu na vitabu kadhaa ambavyo hutungwa na kuandikwa na waandishi wa zama hizi kati ya watunzi wafuatao Madrasa ya Ahlul-Bait (AS), au watunzi ambao Mwenyezi Mungu amewaongoza na kuwapa taufiki kujiunga na madrasa hii tukufu. Mbali na hayo, Jumuiya pia imechukua jukumu la kusambaza na kuyafanyia utafiti mambo yenye faida kwenye tungo na vitabu vya maulama watukufu wa Kishia, wakiweo wa zamani, ili viwe chemchemi ya maji matamu kwa ajili ya kukata kiu ya nafsi zenye kutafuta haki na ukweli. Jambo hilo litawawezesha kufungukiwa na ukweli wa Madrasa ya Ahlul-Bait wa Mtume ulimwengu kote, katika zama hizi ambapo akili ni zenye kukamilika na kupevuka na nafsi na roho kuungana kwa kasi kubwa na kwa kiwango cha kushangaza.

Tunatoa shukurani zetu za dhati kwa mheshimiwa Sayyid Muhammad Hussein Murtadha kwa kuandika kitabu hiki na pia kwa ndugu wote waliochangia, kwa njia moja au nyingine, uchapishaji wake.

Ni matarajio yetu sote kuwa tumefanikiwa, kadiri ya uwezo wetu, kuchangia sehemu ya majukumu yaliyo mabegani kwetu kuhusiana na ujumbe wa Mola wetu Mtukufu ambaye alimtuma Mtume wake kwa uongofu na

dini iliyo ya kweli, ili aidhihirishe juu ya dini zote. Na Mwenyezi Mungu anatosha kuwa Shahidi wa yote.
Jumuiya ya Kimataifa ya Ahlul-Bait (AS)
Kitengo cha Utamaduni

HAJA YA KUSHIRIKIANA NA KUELEWANA

Na tukakufanyeni mataifa na makabila mbali mbali ili mjuane.
Uislamu ulikuja hali ya kuwa mataifa mbali mbali yalikuwa ni yenye kutengana na kugombana. Yalikuwa ni yenye kuzozana na kugombana, lakini kwa kuja Uislamu, ghafla hali ilibadilika na mazingira ya kufahamiana kutawala. Hali ya kubughudhiana na kupingana ilitokomezwa na kuenea hali ya kusaidiana. Ugomvi ulitoweka, na hali ya kushirikiana kuchukua nafasi ya kufanyiana vitimbi. Hayo yote yalitokana na fadhila na ubora wa mafundisho ya Uislamu yenye kuunganisha watu na kuwafanya kuwa kitu kimoja. Matokeo yake yake yalikuwa ni kudhihiri umma mmoja na mkubwa ambao uliwaletea watu utamaduni mkubwa na adhimu. Uliwahami na kuwalinda watu wake kutokana na kila muovu na dhalimu, na hivyo kuufanya uogopewe na kuheshimika mbele ya walimwengu na mataghuti pamoja na watawala wenye kiburi.

Jambo hilo halingewezekana kama usingekuwa ni umoja wa umma huo pamoja na kuungana na kushirikiana watu wake, chini ya kivuli cha Uislamu, licha ya kutofautiana katika rangi, jinsia, ijtihadi, tamaduni na mila. Kwani ilitosha tu kukubaliana katika mambo ya msingi na ya wajibu. Umoja ni nguvu, na utengano ni udhaifu.
Mambo yaliendelea kuwa hivyo hadi pale hali ilipobadilika. Maelewano yalibadilika na kuwa ugomvi na kufahamiana

kukawa kuchukiana. Baadhi ya makundi ya watu yalianza kukufurishana na kupigana wao kwa wao na hivyo kutowesha utukufu na izza yao. Nguvu ya umma huo iliparaganyika na heshima yake kuporomoka. Mataghuti wakaudharau umma ule uliokuwa nembo na mfano wa kuigwa na uliokuwa msitari wa mbele kwa umoja, hadi mmbwa mwitu na mabweha wakajichomeka kwenye safu zake. Walianza kupata satua katika nchi za Kiislamu, watu wenye mitizamo finyu na waliolaaniwa na Mwenyezi Mungu na wasiopendwa na watu. Walipelekea kuporwa utajiri wa Waislamu na kudharauliwa heshima na matukufu yao ya kidini. Katika mazingira hayo, Waislamu walishindwa mara kwa mara na kudhalilishwa jambo lililopelekea ardhi zao kutekwa zikiwemo za Andalusia (Hispania), Bukhara, Samarqand, Tashqand, Baghdad, zamani na hivi sasa, Palestina na Afghanistani.

Ardhi hizo zote ziliomba msaada bila ya kuitikiwa na yoyote yule. Ingewezekana vipi kuitikiwa wakati ugonjwa ulitofautiana kabisa na dawa zilizotolewa kuutibu?! Hakika Mwenyezi Mungu hawezeshi mambo kufanyika ila kupitia sababu zake. Umma huu hautatengenekewa jambo isipokuwa kwa kuzingatiwa mambo yaliyoufanya uwe mwema mwanzoni.

Na hii leo tunashuhudia namna Umma wa Kiislamu unavyolengwa kwa hujuma na mashambulizi ya kinyama zaidi kutoka kwa maadui. Umoja wake unahujumiwa moja kwa moja kupitia uwekaji nyufa kwenye maisha yake ya kimadhehebu na ya kiijitihadi. Mashambulizi haya yanakaribia kutoa matunda yake maovu. Je, si ni jambo la dharura kwa Umma huu kuendelea na juhudi za kuzizatiti

na kuziimarisha safu zake na kuufanya madhubuti uhusiano wa wafuasi wake? Licha ya Umma huu kuwa na madhehebu tofauti, lakini yote yanashirikiana katika Kitabu cha Mwenyezi Mungu na Sunna za Mtume (SAW) vikiwa ni vyanzo vyao muhimu vya sheria na imani, Tawhiid, Utume, Siku ya Mwisho (Akhera), swala, funga, hija, zaka na jihadi katika mambo ya halali na haramu na katika kumpenda Mtume na Ahlul-Bait wake, (rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yao), hata kama huenda kukawa na nguvu na udhaifu fulani miongoni mwa Waislamu kuhusiana na suala hili. Kwa hivyo umma huu ni kama vidole vya mkono mmoja ambavyo licha ya kuwa ni tofauti katika urefu na ukubwa lakini vyote huishia kwenye mkono huohuo mmoja. Au ni kama mwili wa mwanadamu ambao licha ya kuwa na viungo tofauti visivyofanana, lakini vyote hufanya kazi kwa manufaa ya mwili huo mmoja.

Mifano hii ya mkono na mwili wa mwanadamu haiko mbali na ukweli unaopasa kutawala katika Ulimwengu wa Kiislamu.

Maulama wa makundi na madhehebu mbali mbali za Kiislamu huko nyuma, walikuwa wakiishi pamoja bila kugombana wala kuzozana au kupigana, bali walikuwa wakisaidiana na kushirikiana katika muda wote huo. Kwa mfano, mmoja wao akifafanua na kusherehesha kitabu cha mwenzake kutoka madhehebu nyingine ya Kiislamu, kiwe ni cha itikadi au fiqhi, wakienda kusoma na kujifunza kwa wanazuoni wa madhehebu nyingine, wakisifiana, wakiunga mkono rai na nadharia za maulama wengine, wakiwapa wenzao ijaza ya kupokea riwaya za wengine, baadhi wakiwaomba ruhusa wengine kunukuu riwaya kutoka

kwenye madhehebu yao, wakisali nyuma ya wengine na kutambua madhehebu yao na kadhalika. Waislamu hao waliishi pamoja kwa mapenzi na utulivu, kiasi kwamba walionekana ni kana kwamba hawakuwa na tofauti wala utengano wowote. Pamoja na kuwa kulikuwepo na upinzani pamoja na tofauti za mitazamo miongoni mwao, lakini waliweza kuzitatua kwa utulivu na kwa njia za kielimu na kiadabu.

Kuna dalili nyingi zilizo hai na za kihistoria juu ya ushirikiano na usaidianaji huu wa kina na mpana. Kupitia ushirikiano huo, kwa hakika maulama wa Kiislamu waliulimbikizia utajiri mkubwa urithi na utamaduni wa Kiislamu. Kwa kufanya hivyo, walitoa mfano mzuri sana wa kuwepo uhuru wa madhehebu. Hii ni pamoja na kuwa, ushirikiano huo uliwafanya wazingatiwe na kuheshimiwa ulimwenguni.

Kwa hakika, si vigumu kwa maulama wa umma kujumuika na kujadiliana kwa utulivu na kimaudhui, ikhlasi na nia safi, kuhusu mambo yanayozusha tofauti kati ya makundi na madhehebu mbalimbali ya Kiislamu. Kwa kufanya hivyo, kila madhehebu, itapata fursa ya kutoa dalili za kuthibitisha usahihi wake.

Kama ambavyo ni jambo jema na lenye kukubalika kiakili kwamba, kila madhehebu na wafuasi wake wachukue jukumu la kuzitambulisha itikadi na misimamo yao ya kifikra na kifiqhi kwa uhuru na uwazi kamili, ili uweze kubainika ubatili wa tuhuma na shubha zizuliwazo dhidi ya madhehebu au kundi hilo. Kama wanavyofahamu watu wote, vitu vinavyowaunganisha Waislamu ni vingi zaidi kuliko vinavyowatenganisha. Kuthibiti kwa jambo hilo bila shaka

kutasaidia sana katika kuondoa uadui na chuki, na wakati huohuo kuimarisha ushirikiano na udugu miongoni mwa Waislamu.

Kitabu hiki ni sehemu ya hatua za kuelekea kwenye lengo hilo. Kimeandikwa kwa ajili ya kuwabainishia watu ukweli kama ulivyo. Mwenyezi Mungu ndiye mwenye kuwapa taufiki waja wake.

MADHEHEBU YA JAAFARIYYAH IMAMIYYAH

1-Madhehebu hii ya Jaafariyyah Imamiyyah ni madhehebu na kundi kubwa kati ya Waislamu katika zama hizi, na idadi yao inakadiriwa kuwa ni robo ya idadi ya Waislamu wote duniani, na mizizi yao ya kihistoria inafika hadi mwanzoni mwa Uislamu siku ilipoteremka kauli ya Mwenyezi Mungu mtukufu katika Suuratul-Bayyinah isemayo:

ۇۇۋۋۇۇ ىىې

(Hakika wale ambao wameamini na kutenda matendo mema hao ndio viumbe bora).[1]

Basi Mtume wa Mwenyezi Mungu (SAW) akaweka mkono wake juu ya bega la Ali bin Abi Twalib (AS), na huku maswahaba wakishuhudia, akasema:

يَا عَلِيُّ، أَنْتَ وَشِيعَتُكَ هُمْ خَيْرُ الْبَرِيَّةِ.

(Ewe Ali! Wewe na wafuasi wako (mashia wako) ndio viumbe bora zaidi).

(Kama mfano rejea: Tafsirut-Tabariy (Jaamiul-Bayan) na ad-Durrul-Manthuur cha Allamah as-Suyuutwiy mfuasi wa madhehebu ya Shafii, na Tafsiru Ruuhul-Maani cha Aalusiy al-Baghdadiy mfuasi wa madhehebu ya Shafii katika kuifasiri aya hiyo).

Kutokana na aya hii ndio maana kundi hili au madhehebu hii inasibishwayo kwa Imam Jaafar as-Swaadiq (AS) kutokana na kufuata fiqhi yake ikaitwa na kujulikana kwa jina la Shia.

[1]- Suuratul-Bayyinah aya 7.

2-Wafuasi wa madhehebu hii au kundi hilii wanaishi kwa wingi katika nchi za Iran, Iraq, Pakistani, Afghanistani na India. Idadi kubwa ya wafuasi wake pia wameenea katika nchi za Ghuba ya Uajemi, Uturuki, Siria, Lebanon, Urusi na jamhuri zilizojitenge kutoka Urusi. Pia wamesambaa na kutawanyika katika nchi za ulaya kama vile Uingereza, Ujerumani, Ufaransa na Amerika, katika bara la Afrika na katika nchi za Asia Mashariki. Wanayo misikiti na vituo vingi vya kielimu, kiutamaduni na kijamii katika nchi hizo.

3- Na wanatokana na jinsia, vizazi, lugha na rangi mbali mbali, na wanaishi kwa kushirikiana bega kwa bega na ndugu zao Waislamu wafuasi wa makundi na madhehebu mengine katika amani na mapenzi. Wanasaidiana nao katika nyanja zote na katika majali yoyote kwa ukweli na ikhlasi (utakasifu wa moyo) na hufanya hivyo kutokana na kauli ya Mwenyezi Mungu mtukufu isemayo:

ۇ ۋۋ ۋ

(Bila shaka waumini wote ni ndugu).[1]

Na kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu:

(Na saidianeni katika mambo mema na ucha Mungu).[2]

Na kwa kushikamana na kauli ya Nabii Mtukufu (SAW):

الْمُسْلِمُونَ يَدٌ وَاحِدَةٌ عَلَى مَنْ سِوَاهُمْ.

(Waislamu ni sawa na mkono mmoja dhidi ya wasio kuwa Waislamu). [1]

[1]- Suuratul-Hujraat aya 10.
[2]- Suuratul-Maaidah aya 2.

Na kauli yake (SAW):

الْمُؤْمِنُونَ كَالْجَسَدِ الْوَاحِدِ.

(Waumini ni kama mwili mmoja).[2]

4-Na katika muda wote huo wa historia ya Kiislamu walikuwa na misimamo mizuri na yenye kumeremeta katika kuutetea Uislamu na umma mtukufu wa Kiislamu. Kama ambavyo walikuwa na tawala na serikali zilizoutumikia utamaduni wa Kiislamu, na wanazuoni na wanafikra waliotoa mchango mkubwa katika kuutajirisha urithi wa Kiislamu kwa kutunga mamia kwa maelfu ya vitabu. Vitabu vikubwa na vidogo katika nyanja za tafsiri ya Qur'an na hadithi, itikadi, fiqhi na usuli, akhlaq (maadili), diraya na rijali, falsafa na mawaidha, utawala na jamii, lugha na fasihi. Bali waliandika kuhusu tiba pia, fizikia na kemia, hesabu na elimu nujumu na elimu nyingine zinazohusiana na maisha. Walikuwa na nafasi kubwa na ya msingi katika ufumbuzi wa elimu nyingi (rejea kitabu: Taasisu Shia Liuluumil-Islaami, cha Swadr, na al-Dhariah ilaa Taswaanifi Shiah cha Agha Buzorgi (chenye juzuu 29) na Kashfu Dhunuun cha Afandi na Muujamul-Muallifiin cha Kahaalah, na Aayanush-Shiah cha Sayyid Muhsin al-Amiin al-Aamuliy, na wengineo).

5- Wanamuitakidi na kumuamini Mungu mmoja wa pekee na mpweke mwenye kutegemewa, ambaye hakuzaa wala kuzaliwa, na wala hakuna yeyote aliye mfano wake. Hupinga suala la Mwenyezi Mungu kuwa na mwili, mahali au sehemu maalumu na wakati, na hupinga kubadilika na kugeuka na

[1]- Musnad Ahmad juzu 1 \ 215.
[2]-Al-bukhariy, kitabul-adabi: 27.

kuwa na harakati na kupanda juu, kuteremka na mengine yasiyokuwa hayo kati ya mambo yasiyowiana na utukufu wa Mwenyezi Mungu na utakasifu wake wala ukamilifu na uzuri wake.

Na wanaitakidi ya kuwa yeye Mwenyezi Mungu ndiye tu mwenye kuabudiwa na hakuna mwinginewe anayestahili kuabudiwa, na kwamba hukumu na uwekaji wa sheria ni wake peke yake na si mwinginewe, na kwamba shirki na aina zake zote na rangi zake, zilizofichika na zilizo wazi, ni dhulma kubwa na dhambi isiyosameheka.

Na yote haya huyachukua kutoka kwenye akili safi iungwayo mkono na Kitabu Kitukufu, na Sunna tukufu iliyo sahihi bila ya kujali chanzo chake.

Na katika nyanja za itikadi hawachukui hadithi za kiisraili (zilizopokelewa kwenye Taurati na Injili) na za kimajusi ambazo humpa Mwenyezi Mungu Mtukufu maumbile na sura ya mtu, na kumfananisha na viumbe alivyoumba mwenyewe.

Au zinazomnasibisha na uovu, kiburi, dhulma, kufanya upuuzi na kufanya vitu bila malengo. Ametakasika Mwenyezi Mungu na hayo utakasifu mkubwa.

Au zinazowanasibisha mitume watwaharifu na madhambi makubwa na matendo mabaya, mitume walio maasumu katika matendo yao yote.

6- Wanaitakidi ya kwamba, Mwenyezi Mungu mtukufu ni muadilifu na mwenye hekima. Ameumba kwa uadilifu na hekima, na hakuumba kitu chochote kwa upuuzi, kiwe ni kitu kisicho na roho au mmea, awe mnyama au mwanadamu, iwe mbingu au ardhi, kwa sababu upuuzi na

kutokuwa na malengo kunapingana na uadilifu na hekima, na hayo yanapingana na uungu ambao unalazimika kuthibitisha ukamilifu wote kwa Mwenyezi Mungu mtukufu, na kupinga apungufu wa aina yoyote kwake Mwenyezi Mungu Mtakasifu.

7- Wanaitakidi ya kuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu aliwatumia viumbe - kutokana na uadilifu na hekima yake- tangu walipoanza maisha yao duniani- manabii na mitume, waliosifika kwa sifa ya Ismah (walioepushwa na dhambi) na wakapambika kwa elimu kubwa na pana, waliopewa- kupitia njia ya ufunuo (wahyi)- kutoka kwa Mwenyezi Mungu, na kwa malengo ya kuwaongoza viumbe, na kuwasaidia kuweza kufika kwenye ukamilifu utakiwao, na kuwaongoza kwenye utiifu ambao utawapelekea kuingia peponi, na kuwaandaa kwa ajili ya kupata rehma ya Mwenyezi Mungu na radhi zake. Walio maarufu zaidi kati ya manabii na mitume hawa ni:
Adam, Nuhu, Ibrahiim, Isa, Musa na wengineo wasio kuwa hawa kati ya mitume waliotajwa na Qur'an Tukufu au waliotajwa na kuelezewa kwenye hadithi tukufu.
8- Wanaitakidi ya kuwa mwenye kumtii Mwenyezi Mungu, na kutekeleza amri zake na kutekeleza kanuni zake kimatendo katika nyanja tofauti za maisha atakuwa amefaulu na kuokoka, na atastahili kusifiwa na kupata thawabu, hata kama atakuwa ni mtumwa wa Uhabeshi, na kwamba mwenye kumuasi Mwenyezi Mungu mtukufu na kujisahaulisha amri zake, na akatekeleza amri zingine zisizo kuwa za Mwenyezi Mungu Mtukufu, atakuwa amepata hasara na ni mwenye kuangamia na atastahili kukemewa na

kupata adhabu na mateso, hata kama atakuwa ni bwana na sayyid wa Kikuraishi, kama ilivyokuja na kuelezwa katika hadithi ya Mtume Mtukufu (SAW).
Wanaitakidi kuwa mahala pa kupewa thawabu na adhabu ni Siku ya Kiama (Siku ya Hukumu) siku ambayo itatokea baada ya kupita na kuvuka kwenye ulimwengu wa kaburi na Barzakh. Hata hivyo, wanapinga tanaasukh (kuhamishiwa roho za wafu kwenye viwiliwili vigine vipya) jambo ambalo huaminiwa na kuitakidiwa na watu wenye kupinga ufufuo, kutokana na kuwa linapingana moja kwa moja na Qur'an Tukufu na Sunna twaharifu.

9- Na wanaitakidi kuwa Nabii na Mtume wa mwisho, na mmbora wao ni Mtume wa Mwenyezi Mungu Muhammad bin Abdillahi bin Abdil-Mutwalib (SAW)[1] ambaye Mwenyezi Mungu alimuhifadhi kutokana na makosa na kuteleza, na kumuhifadhi na maasi makubwa na madogo, kabla ya utume na baada yake, katika mambo ya kufikisha ujumbe na mengineyo, na akateremsha kwake Qur'an tukufu, ili iwe ndiyo katiba ya maisha ya viumbe hadi milele, na Mtume (SAW) kufikisha ujumbe na kutekeleza amana kwa ukweli na ikhlasi (utakasifu wa moyo), na akatoa katika njia hii kilicho ghali na rahisi (yaani kila alichokimiliki katika njia hii).
Katika nyanja za uandishi wa historia ya Mtume (SAW), shakhsia, historia, sifa zake za pekee na miujiza yake, Mashia

[1]-Mashia Imamiyyah wanaitakidi kuwa ni lazima kuwataja kizazi chake mtume pamoja na jina lake wakati wa kumswalia, kutokana na amri yake (SAW) kufanya hivyo kama ilivyokuja na kuelezwa katika baadhi ya vitabu Sahihi na vinginevyo.

wana tungo na vitabu vingi. (Ili kuvifahamu rejea kwenye: Kitaabul-Irshaad cha Shekh Mufiid, na Aalaamul-Waraa Biaalamul-Hudaa cha Twabarsiy, na Mausuuatu Biharul-An'waar cha Majlisiy, na Mausuatur-Rasulil-Mustafa cha Sayyid Muhsin al-Khatamiy kilichoandikwa hivi karibuni).

10- Wanaitakidi kuwa Qur'an Tukufu, ambayo iliteremshwa kwa Mtume wa Uislamu Muhammad (SAW) kupitia kwa Jibrilu Muaminifu, na kuandikwa na kundi fulani la maswahaba wakubwa na wakitanguliwa au kuongozwa na Ali bin Abi Twalib (AS) katika zama za Mtume Mkarimu Muhammad (SAW), na chini ya uangalizi na usimamizi wake na kwa amri yake na maelekezo yake, na wakaihifadhi nyoyoni na kuifahamu fika, na kuhesabu hadi herufi zake na maneno yake, sura zake na aya zake, na kunukuliana zama baada ya zama, ndiyo isomwayo na Waislamu wote pamoja na madhehebu zao katika zama za leo. Ndiyo Qur'an hiyohiyo waisomayo usiku kucha na mchana kutwa, bila ya kuzidi wala kupungua, au kupotoshwa au kubadilishwa. Mashia katika nyanja hizi wanavyo vitabu vingi vilivyoandikwa kwa njia ya muhtasari na pia kwa upana sana.
(Ili kujua zaidi rejea kitabu: Taarikhul-Qur'an cha Zanjaniy, na Tamhiid fii Ulumil-Qur'an cha Muhamma Haadiy Maarifat, na vinginevyo visivyo kuwa hivi).

11- Wanaitakidi kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu Muhammad (SAW) pindi ulipowadia wakati wa kufariki kwake dunia alimsimamisha na kumsimika Ali bin Abi Twalib awe khalifa wake na Imam wa Waislamu baada yake, ili awaongoze kisiasa, kifikra, atatue matatizo yao na aendeleze kazi ya kuwalea na kuwatakasa. Hilo lilifanyika

kwa amri ya Mwenyezi Mungu mtukufu katika sehemu au mahali paitwapo (Ghadir Khum), mwishoni mwa maisha yake, na katika hija yake ya mwisho, katika mkusanyiko mkubwa wa Waislamu waliohiji pamoja naye, na ambao baadhi ya riwaya zinasema kuwa walikuwa ni watu laki moja. Kwa hakika katika mnasaba huu, ziliteremka aya nyingi.[1]

Kama ambavyo Mtume (SAW) aliwataka watu kumpa baia Ali kwa kupeana naye mkono, na watu kumpa baia wakitanguliwa na viongozi wa Muhajiriina na Answari na maswahaba mashuhuri na maarufu (rejea kitabu al-Ghadiir cha Allamah al-Aminiy akinukuu kutoka kwenye vyanzo vingi vya Kiislamu vya tafsiri na historia).

12- Na wanaitakidi kuwa Imam- baada ya Mtume wa Mwenyezi Mungu Muhammad (SAW)- kama ambavyo

[1]-Aya hizo ni hizi zifuatazo: Kauli yake Mwenyezi Mungu isemayo: Ewe Mtume! Fikisha yale uliyoteremshiwa kutoka kwa mola wako na kama hukufanya basi utakuwa hukufikisha ujumbe Wake na Mwenyezi Mungu atakulinda na watu hakika Mwenyezi Mungu hawaongozi watu makafiri). (Suuratul-Maaidah aya 67).
Na kauli yake Mtukufu katika aya ya kukamilisha dini isemayo: (Hivi leo nimekukamilishieni dini yenu na nimezitimiza juu yenu neema zangu na nimeridhia kwenu Uislamu kuwa ndiyo dini ya kweli) (Suuratul-Maaidah aya 3).
Na kauli yake Mtukufu: Hivi leo wale waliokufuru wamekata tamaa kutokana na dini yenu kwa hivyo basi msiwaogope na niogopeni mimi). (Suuratul-Maaidah aya 3).
Na kauli yake Mtukufu: Aliomba muombaji adhabu iliyotokea* kwa ajili ya makafiri hana wa kumuepusha na adhabu hiyo). (Suuratul-Maariji aya 2).

ulikuwa ni wajibu kutekeleza yale aliyokuwa akiyatekeleza Mtume (SAW) katika maisha yake kama vile uongozi na muongozo, na malezi na mafunzo, na kubainisha au kufafanua hukumu, na kutatua matatizo ya kifikra yaliyokuwa mazito kwa watu wa kawaaida, na kutatua matatizo na mambo ya kijamii yaliyo muhimu, itakuwa ni lazima kwake (Imam na khalifa baada ya Mtume) awe katika hali ambayo watu watakuwa na matumaini naye, ili aweze kuuongoza umma hadi kwenye ukingo wa amani, kwani yeye hushirikiana na Mtume katika maandalizi na sifa zote, (na kati ya hizo ni kuwa maasum na kuwa na elimu pana) kwa sababu yeye anashirikiana naye katika mambo yote na majukumu yote ukitoa suala la kupokea ufunuo (wahyi) na utume. Hii ni kwa sababu utume ulimalizika na kukomea kwa Muhammad bin Abdillahi (SAW). Yeye ni nabii wa mwisho, na mwisho wa mitume. Dini yake ni dini ya mwisho, sheria yake ni sheria ya mwisho na kitabu chake ni kitabu cha mwisho. Hakuna nabii, dini wala sheria nyingine baada ya sheria yake. (Mashia katika nyanja hizi wanavyo vitabu vingi na vya aina mbali mbali kwa ukubwa na mfumo).

13- Wanaitakidi kuwa umma kumuhitajia kiongozi mwema, na walii aliye maasum kulilazimu kutotosheka na kuteuliwa kwa Ali (AS) peke yake ili kuchukua cheo cha ukhalifa na Uimamu baada ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (SAW), bali hapakuwa na budi ya silsila hii ya uongozi kuendelea kwa muda mrefu, hadi mizizi ya Uislamu iweze kujizatiti, misingi ya sheria kuhifadhiwa na kanuni zake kulindwa kutokana na hatari ambazo zilitishia na zinasotishia kuiangamiza itikadi ya Mungu na kila nidhamu ya Mola.

Jambo hili lilipaswa kutimia ili kundi la Maimamu liweze kuupatia Umma- kutokana na yale wayatekelezayo kama vile nafsi zao mbali mbali na matendo yao tofauti katika mazingira ya aina mbali mbali- mifano hai ya kimatendo na mipango munasibu na inayonasibiana na hali zote ambazo zitaupitia na kupambana nazo umma wa Kiislamu katika siku za baadaye.

14- Wanaitakidi kwamba Mtume Muhammad bin Abdillah (SAW) kutokana na sababu hii na kutokana na hekima hii ya hali ya juu kabisa, aliwateua kwa amri ya Mwenyezi Mungu Mtukufu maimamu kumi na mmoja baada ya Imam Ali (AS) - wakiungana pamoja na Ali- wanakuwa maimamu kumi na wawili. Zimepokelewa habari ziashiriazo idadi yao, na kabila lao (Kuraishi)- na sio majina yao na sifa zao mahususi- katika Sahihi Bukhari na Muslim kwa lafdhi tofauti. Wamepokea mabwana hao wawili hadithi kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (SAW), ya kwamba dini itaendelea kuwepo au kusimama au yenye tukufu na yenye kuwazuwia maadui kwa muda watakaokuwepo maamiri kumi na wawili, au makhalifa, wote wakitokana na kabila la Kikuraishi, (au katika famili ya bani Haashim, kama ilivyopokelewa katika baadhi ya vitabu. Majina yao yametajwa katika vitabu vingine visivyokuwa Sahihi Muslim na Bukhari kati ya vitabu vya Fadhaail na Manaaqib na mashairi na fasihi).

Na hadithi hizi hata kama hakutaja moja kwa moja majina ya maimam kumi na wawili, ambao ni Ali na wengine kumi na mmoja watokanao na kizazi chake, lakini ukweli ni kwamba hadithi hizo hazinasibiani na kuwiana ila na yale

wanayoyaitakidi Mashia Jaafariyyah, na hakuna tafsiri sahihi ya hadithi hizo isipokuwa ile wanayoitoa wao kuhusiana na jambo hilo. (Ili kuelewa zaidi rejea kitabu: Khulafaun-Nabii, cha Haairiy al-Bahraniy).

15- Mashia Jaafariyyah wanaitakidi kwamba Maimamu kumi na wawili ni hawa wafuatao: Imam Ali bin Abi Twalib (mtoto wa ami yake Mtume wa Mwenyezi Mungu na mkwewe kwa binti yake Zahraa (AS).
Imam Hassan na Imam Husein (watoto wawili wa Ali na Fatuma (AS), na wajukuu wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (SAW)).
Imam Zainul-Abidiin Ali bin Hussein (as-Sajjad) (AS)
Imam Muhammad bin Ali (al-Baaqir)
Imam Jaafar bin Muhammad (as-Swaadiq).
Imam Musa bin Jaafar (al-Kaadhim).
Imam Ali bin Musa (ar-Ridhaa).
Imam Muhammad bin Ali (al-Jawaad at-Taqii).
Imam Ali bin Muhammad (al-Hadiiy an-Naqii).
Imam Hasan bin Ali (al-Askariy).
Imam Muhammad bin Hasan (al-Mahdi al-Maw'uud al-Muntadhar).[1]

[1]-Na kwa hakika wanalugha wa aina yake wasio Mashia-kati ya Waarabu na wasio Waarabu- walitunga na kuandika kaswida kubwa na pana ambazo zilikuwa na majina ya maimamu kumi na wawili wote kama vile Haskafiy na Ibnu Tuuluun na Al-fadhli bin Ruuzbahaar na al-Jaamiy na al-Atwaar an-Naishaburiy na Mawlawiy, na hao ni miongoni mwa wafuasi wa madhehebu ya Hanafi na Shaafii'i na mengineyo, Tutataja kama mifano hai kaswida mbili kati ya kaswaida hizo:
Ya kwanza: Kaswida ya Haskafiy mfuasi wa madhehebu ya Hanafii, naye ni miongoni mwa wanazuoni wa karne ya sita Hijiria, anasema katika kaswid hiyo:

حَيْدَرَةٌ وَالْحَسَـــنَانِ بَعْـــدَهُ ثُمَّ عَلِـــيٌّ وَابْنُـــهُ مُحَمَّـــدُ

Na kwamba hawa ndio Ahlul-Bait ambao waliwekwa na kusimikwa na Mtume wa Mwenyezi Mungu Muhammad (SAW) - na kwa amri kutoka kwa Mwenyezi Mungu- kuwa ni viongozi wa Umma wa Kiislamu, kutokana na isma yao, na kuwa kwao watwaharifu kutokana na makosa na madhambi, na kutokana na elimu yao pana ambayo waliirithi kutoka kwa babu yao- na kuamuru kuwapenda na kuwafuata, pale aliposema Mwenyezi Mungu mtukufu:

وَجَعْفَرُ الصَّادِقُ وَابْنُ جَعْفَرٍ مُوسَى وَيَتْلُوهُ عَلِيُّ السَّـــيِّدُ
أَعْنِي الرِّضَا ثُمَّ ابْنُهُ مُحَمَّـــدٌ ثُمَّ عَلِـــيٌّ وَابْنُـــهُ الْمُسَـــدَّدُ
الْحَسَنُ التَّالِي وَيَتْلُو تِلْـــوَهُ مُحَمَّدُ بنُ الْحَسَنِ الْمُعْتَقَـــدُ
قَوْمٌ هُمُ أَئِمَّتِـــي وَسَـــادَتِي وَإِنْ لَحَانِي مَعْشَرٌ وَفَنَّـــدُوا
أَئِمَّـــةٌ أَكْـــرِمْ بِهِـــمْ أَئِمَّـــةً أَسْمَاؤُهُمْ مَسْرُودَةٌ لاَ تُطْـــرَدُ
هُمْ حُجَجُ اللهِ عَلَى عِبَـــادِهِ وَهُمْ إِلَيْهِ مَـــنْهَجٌ وَمَقْصَـــدُ
هُمُ النَّهَـــارَ صُـــوَّمٌ لِـــرَبِّهِمْ وَفِي الدَّيَاجِي رُكَّعٌ وَسُـــجَّدُ

Na kaswida ya pili: ni ya Shamsud-din Muhammad bin Tuuluun kati ya wanazuoni wa karne ya kumi hijiria, naye anasema katika kasida hiyo:

عَلَيْكَ بِالأَئِمَةِ الإِثْنَـــيْ عَشَـــرْ مِنْ آلِ بَيْتِ الْمُصْطَفَى خَيْرِ الْبَشَرْ
أَبُو تُـــرَابٍ حَسَـــنٌ حُسَـــيْنُ وَبُغْـــضُ زَيْـــنِ الْعَابِـــدِينَ شَـــيْنُ
مُحَمَّدُ الْبَاقِرُ كَمْ عِلْـــمٌ دَرَى وَالصَّادِقُ ادْعُ جَعْفَراً بَيْنَ الْـــوَرَى
مُوسَى هُوَ الْكَاظِمُ وَابْنُهُ عَلِـــي لَقَبُـــهُ الرِّضَـــا وَقَـــدْرُهُ عَلِـــي
مُحَمَّدُ التَّقِـــيُّ قَلْبُـــهُ مَعْمُـــورُ عَلِـــيُّ النَّقِـــيُّ دُرُّهُ مَنْثُـــورُ
وَالْعَسْكَرِيُّ الْحَسَنُ الْمُطَهَّـــرُ مُحَمَّدُ الْمَهْـــدِيُّ سَـــوْفَ يَظْهَـــرُ

Rejea kitabu: al-Iimmatul-Ithna Ashara, kilichoandikwa na mwanahistoria wa Damascus Shamsud-din Muhammad bin Tuuluun aliyefariki mwaka 953 hijira, kilichohakikiwa na: Dr. Swalaahud-dini al-Munjjad. Chapa ya Beirut.

ﭖ ﭗ ﭘ ﭙ ﭚ ﭛ ﭜ ﭝ

(Sema: Sikutakeni malipo juu ya kazi ya kuufikisha Uislamu isipokuwa kuwapenda watu wangu wa karibu (jamaa zangu).[1]

Na Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

ﭺ ﭻ ﭼ ﭽ ﭾ ﭿ ﮀ ﮁ ﮂ ﮃ

(Enyi mlioamini! Mcheni Mwenyezi Mungu na kuweni pamoja na wakweli).[2]

(Rejea vitabu vya hadithi, tafsiri na fadhila vilivyomo ndani ya vitabu vikubwa kama vile Sahihi Muslim na Bukhari na vyenye kujitegemea katika madhehebu kuu mbili).

16- Shia Jaafariyyah wanaitakidi kwamba, Maimamu hawa watwaharifu ambao historia haikuandika wala kusajili juu yao jambo lolote la kuteleza au dhambi, katika kauli na matendo yao, kuwa hakika waliutumikia- kwa elimu yao- Umma wa Kiislamu, na kuutajirisha utamaduni wao kwa maarifa ya kina, na mtazamo sahihi katika uwanja wa itikadi, sheria, akhlaq na adabu, tafsiri, historia na mtazamo wa mustakbali.

Kama walivyosimamia kazi ya kulea- kwa mfumo wa kikauli na kimatendo- kundi la wanaume na wanawake wa aina ya pekee na wateule walio wema ambao watu wote walikiri juu ya fadhila, elimu na sera yao nzuri.

Wanapokea na kusimulia kwamba wao hata kama walitengwa-kwa masikitiko makubvwa- na kuwekwa mbali na cheo cha uongozi wa kisiasa- lakini ukweli ni kwamba walitekeleza ujumbe wao wa kifikra na kijamii vyema kama

[1]-Suuratu Shuraa aya 23.

[2]-Suuratut-Tawbah aya 119.

ilivyotakiwa, kwani walihifadhi na kulinda vyanzo vya itikadi, na kanuni za kisheria kutokana na makosa.

Na lau kama Umma wa Kiislamu ungewapa nafasi ya kutekeleza ipaswavyo jukumu lao kisiasa ambalo walipewa na Mtume wa Mwenyezi Mungu (SAW) kwa amri ya Mwenyezi Mungu Aliyetakasika, basi Umma wa Kiislamu ungepata saada, izza na utukufu wake kamili. Ungebakia kuwa ni wenye umoja, wenye kukubaliana na wenye mshikamano usio na mfarakano ndani yake. Kusingekuwepo na tofauti, ugomvi, mapigano, mauaji na kuchinjana na kusingekuwepo na udhalili wala kusaghirika.

(Rejea kwa upana zaidi katika uwanja huu kitabu kifuatacho: al-Imamus-Swadiq Wal-Madhaahibil-Arbaah cha Asad Haidar-ambacho kina juzuu 3- na vinginevyo).

17-Wanaitakidi kwamba- kutokana na sababu hii, na kutokana na dalili za kunukuu na za kiakili ambazo nyingi zimetajwa katika vitabu vya itikadi- ni wajibu kuwafuata Ahlul-Bait, na kushikamana na njia yao bila kuachana nayo, kwa sababu ndiyo njia ambayo ilichorwa na kuwekwa na Mtume wa Mwenyezi Mungu (SAW) kwa ajili ya Umma, na kuusia kuifuata njia hiyo na kushikamana nayo, katika hadithi ya vizito viwili iliyo mutawaatir kwani alisema katika hadithi hiyo:

إِنِّي تَارِكٌ فِيكُمُ الثَّقَلَيْنِ؛ كِتَابَ اللهِ وَعِتْرَتِي أَهْلَ بَيْتِي، مَا إِنْ تَمَسَّكْتُمْ بِهِمَا لَنْ تَضِلُّوا أَبَداً.

(Hakika mimi nimeacha miongoni mwenu vitu viwili vizito, Kitabu cha Mwenyezi Mungu na kizazi changu Watu wa Nyumbani kwangu (Ahlul-Bait wangu), vitu ambavyo ikiwa mtashikamana navyo hamtapotea kamwe baada yangu).

Kama ilivyopokelewa na Muslim katika Sahihi yake na wengineo kati ya mamia ya wasimulizi na wanazuoni katika karne zote za Kiislamu, (Rejea Risaalatul-Hadiithi at-Thaqalaini cha al-Washniy ambacho kilithibitishwa na al-Azhar tukufu kabla ya miongo mitatu takriban).
Kwa hakika suala hili la kuteuliwa khalifa na kutolewa wasia lilikuwa ni jambo la kawaida na lililoenea katika maisha ya mitume waliotangulia. (Rejea: Ithbatul-Waswiyyah cha Masoud, na vitabu vya hadithi, tafsiri na historia vya madhehbu hizi mbili za Shia na Sunni).

18- Shia Jaafariyyah wanaitakidi kwamba ni juu ya Umma wa Kiislamu - Mwenyezi Mungu auenzi na kuutukuza- kuyafanyia mazungumzo na utafiti mambo haya, huku wakiwa wamejiweka mbali na matusi, dhana mbaya, kutuhumiana, vitisho (fazaa) na bila kutatizana katika maneno. Wanazuoni na wanafikra kutoka kwenye madhehebu na makundi yote ya Kiislamu wanapasa kukusanyika na kujumuika katika makongamano ya kielimu, na kudurusu kwa uwazi, ikhlasi, udugu na kimaudhui wayasemayo ndugu zao Mashia Jaafariyyah, na dalili wazisimamishazo juu ya nadharia na muono wao, kwa msingi wa Kitabu na Sunna sahihi za Mtume wa Mwenyezi Mungu (SAW), zilizo mutawaatir, akili salama na misingi ya kihistoria pamoja kuzingatia masuala ya kisiasa na kijamii kwa ujumla yaliyokuwa yakitawala katika zama za Mtume wa Mwenyezi Mungu (SAW) na baada yake.

19- Shia Jaafariyyah wanaitakidi kwamba, maswahaba, wanaume pia wanawake walio kuwa pembezoni mwa

Mtume wa Mwenyezi Mungu (SAW), waliutumikia Uislamu, na kutoa nafsi na kila kilicho cha thamani katika njia ya kueneza na kuizatiti njia na dini ya Kiislamu, na kwamba ni juu ya Waislamu kuwaheshimu, na kuithamini huduma zao walizotoa, na kuwatakia radhi.
Hata hivyo, hili halina maana kuwa wote ni waadilifu moja kwa moja, na kwamba wana nafasi ya juu inayowafanya wasiweze kukosolewa baadhi ya misimamo na matendo yao. Hilo ni kutokana na kwamba, wao ni viumbe wanakosea na kusibu, na historia imethibitisha kwamba baadhi yao walitoka kwenye njia ya sawa hata katika zama za Mtume wa Mwenyezi Mungu (SAW), bali hata Qur'an Tukufu imesema wazi kuhusiana na hilo katika baadhi ya sura na aya zake kama vile Suuratul-Munafiqiin, Ahzaab, al-Hujraati, Tahriim, al-Fat'h, Muhammad na at-Tawbah.
Ukosoaji ulio salama wa misimamo ya baadhi ya maswahaba hao hauna maana ya kufru, kwa sababu vigezo vya imani na kufru viko wazi. Mihimili ya mambo mawili hayo yaani imani na kufru imewekwa wazi nayo ni kuthibitisha au kupinga upweke na ujumbe wa Mwenyezi Mungu, na mambo mengine ya dharura katika katika dini, kama vile wajibu wa swala, funga na hija na uharamu wa pombe, kamari na mfano wa hayo.
Naam, ni wajibu kuhifadhi ulimi kutokana na matusi kwani hayo si katika mambo yanayofaa kufanywa na Muislamu aliyelelewa kimaadili, mwenye kufuata mwenendo na sera za Mtume wa Mwisho Muhammad (SAW). Pamoja na hayo, hakika maswahaba wengi ni wema na wenye kuwaelekeza na kuwaongoza waja, wanaostahili kuheshimiwa na kukirimiwa.

Na kwamba kuwasimamisha mbele ya kanuni za jarhi na taadili (kanuni zenye kuangali kwa makini historia yao na usafi wa mienendo yao) ni kwa ajili tu ya kufahamu na kuelewa sunna sahihi za Mtume na zenye kutegemewa. Hii ni kwa kuzingatia kuwa uongo na uzushi ulifanyika dhidi ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (SAW) baada ya kuaga kwake dunia- kama watu wote wanavyofahamu. Kwa hakika Mtume (SAW) alitoa habari yeye mwenyewe kuhusiana na kutokea kwa uongo huo - na hilo ndio jambo lililowapa nguvu maulama wa madhehebu hizi mbili kama vile Suyuutwiy na Ibnul - Jawaziy na wengineo kutunga vitabu madhubuti vya kutenganisha kati ya hadithi zilizotoka kweli kwa Mtume Mtukufu (SAW) na hadithi zilizopandikizwa na kuzuliwa dhidi yake.

20- Shia Jaafariyyah wanaitakidi kuwepo kwa Imam al-Mahdiy mwenye kungojewa, kutokana na riwaya nyingi zilizopokelewa kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (SAW) ya kwamba, atatokana na kizazi cha Fatuma, na kwamba yeye ni wa tisa kati ya kizazi cha Husein (AS), na kutokana na ukweli kuwa mtoto wa nane wa Husein (AS) ni Imam Hasan al-Askariy na alifariki mwaka 260 hijiria, na hakuwa isipokuwa na mtoto mmoja aliekuwa akiitwa kwa jina la (Muhammad) basi huyo ndiye Imam al-Mahdi mwenye kunia ya Abil-Qaasim.[1] Kwa hakika kuna walio

[1]- Na katika viatabu Sahihi na vinginevyo kati ya vitabu vya madhehebu mbili ni kwamba Mtume (SAW) alisema: Atadhihiri katika zama za mwisho mtu atokanaye na kizazi changu jina lake ni sawa na jina langu na kunia yake ni sawa na kunia yangu ataijaza ardhi kwa uadilifu na usawa kama ilivyojaa dhuluma na ujeuri.

muona kati ya Waislamu waaminifu na kutoa habari za kuzaliwa kwake na sifa zake za pekee, na wakaelezea kuhusu uimamu wake na dalili juu yake kutoka kwa baba yake. Kwa hakiki alifichika na kughibu kunako macho baada ya miaka mitano tangu kuzaliwa kwake, kwa sababu maadui walitaka kumuua na kumuangamiza. Mwenyezi Mungu alimuhifadhi na madhara hayo kwa sababu alitaka kumuandalia nafasi ya kusimamisha dola la Kiislam lenye uadilifu litakaloenea dunia nzima katika Akhiruz-Zaman, na kuitwahirisha ardhi kutokana na dhulma na ufisadi baada ya kujawa na vitu hivyo.

Na hakuna la kushangaza, kama ambavyo hakuna sababu ya kustaajabu, kutokana na umri wake kuwa mrefu, kwani Qur'an imetaja kwamba Masihi (AS) yu hai hadi hivi leo pamoja na kupita miaka 2007 tangu kuzaliwa kwake kutukufu. Nuhu (AS) pia aliishi kati ya kaumu yake miaka elfu moja ila khamsini (950) akiwaita na kuwalingania kwenye njia ya Mwenyezi Mungu, na vile vile Khidhri (AS) bado yu hai.

Kwa hivyo Mwenyezi Mungu ni muweza juu ya kila kitu, na utashi wake ni wenye kutekelezeka hakuna wa kuuzuia wala kuupinga. Je, hakusema kuhusiana na Mtume Yunus (AS):

ﷺ ﷺ ﷺ ﷺ ﷺ ﷺ ﷺ ﷺ ﷺ ﷺ

(Lau kama asingekuwa miongoni mwa wenye kumtakasa na kumsabihi Mwenyezi Mungu* Basi angebakia na kukaa tumboni mwake hadi siku watakapofufuliwa.[1]

[1]-Suuratus-**S**waffaat aya 143-144.

Na kwa hakika maulama watukufu na wakubwa wa Ahli Sunna walikiri kuzaliwa kwa Imam Mahdiy (AS) na kuwepo kwake, na wakataja jina la baba yake na sifa zake kwa mfano:

a. Abdul-Muumin as-Shablanjiy al-Shafiiy katika kitabu chake: Nurul-Abswaar fii Manaaqibi Aali Baitin-Nabiyyil-Mukhtar.
b. Ibnu Hajar al-Haitamiy al-Makkiy al-Shafiiy katika kitabu chake: As-Swaaiqul-Muhriqah kwani alisema kwenye kitabu hicho kutoka kwake: Abul-Qaasim Muhammad al-Hujjah na umri wake wakati alipofariki baba yake ulikuwa ni miaka mitano (5), lakini Mwenyezi Mungu alimpa hekima katika umri huo na kuitwa kwa jina la al-Qaaimul-Muntadhar (aliyesimama na mwenye kungojewa).
c. Al-Qanduuziy al-Hanafiy al-Balkhiy katika kitabu chake: Yanabiiul-Mawaddah kilichochapishwa katika mji wa al-Ustanah ulioko Uturuki katika siku za utawala (ukhalifa) wa Othumaniyyah.
d. Sayyid Muhammad Swadiiq Hasan al-Qanuujiy al-Bukhariy katika kitabu chake: al-Idhaa'ah limaa Kaana wama Yakuunu Baina Yadais-saa'ah. Huyu ni miongoni mwa maulama wa zamani waliotangulia (Mutaqaddi-miin).

Na Miongoni mwa Muta'akhiriin (waliofuatia baadaye) ni Dr. Mustafa Ar-Raafi'ii katika kitabu chake: Islaamuna, kiasi kwamba alizungumzia mas'alah ya kuzaliwa kwa kuyaelezea kwa upana, na kujibu ishkali na pingamizi zote zilizotolewa katika uwanja huu au kuhusu maudhui hii.

21- Shia Jaafariyyah wanaswali, kufunga, kutoa zaka na kutoa khumsi za mali zao, wanakwenda kufanya hija kwenye nyumba tukufu ya Mwenyezi Mungu huko Makkah, wanatekeleza ibada ya umrah na hija katika umri mara moja ikiwa ni wajibu, na zaidi ya mara moja ikiwa ni sunna, wanaamrisha mema na kukataza mabaya, wanawatawalisha mawalii wa Mwenyezi Mungu na mawalii wa Mtume wake, wanawafanyia uadui na kuwachukia maadui wa Mwenyezi Mungu na maadui wa Mtume wake, wanampiga jihadi katika njia ya Mwenyezi Mungu kila kafiri au mshirikina autangaziaye vita Uislamu, na kila mwenye kuufanyia Uislamu hila na vitimbi na njama za kuushambulia umma wa Kiislamu, hutekeleza harakati zao za kiuchumi na za kijamii na kifamilia kama vile biashara ukodishaji kuoa kutaliki urithi na malezi kunyonyesha na mas'ala ya hijab na mengineyo kwa mujibu wa sheria aali za Kiislamu. Huchukua na kutekeleza sheria hizo- kupitia njia ya ijtihadi ambayo huitekeleza wanazuoni wa fiqhi walio wacha Mungu na wenye kujiepusha na dunia,-wakizitoa kwenye Kitabu cha Mwenyezi Mungu na sunna sahihi, na hadithi za Ahlul-Bait zilizothibiti kutoka kwao, na akili na Ijmai ya wanazuoni.

22-Na wanaona ya kuwa kila faradhi kati ya faradhi za kila siku ina wakati maalumu, na kwamba nyakati za swala za kila siku ni tano: (Alfajiri, Adhuhuri, Alasiri, Maghribi na Ishaa). Na kwamba kilicho bora ni kuitekeleza kila sala katika wakati wake maalumu, isipokuwa ni kwamba wao wanakusanya kati ya swala mbili za Adhuhuri na Alasiri, na kati ya Maghribi na Ishaa, kwa sababu Mtume wa Mwenyezi Mungu (SAW) alikuwa akikusanya na kujumuisha kati ya swala mbili hizo bila ya kuwepo na udhuru wala ugonjwa

wala mvua wala safari- kama ilivyopokelewa katika Sahihi Muslim na vitabu vinginevyo- kwa ajili ya kuufanyia umma wepesi, na kuusahilishia, na hilo ni jambo la kawaida katika zama zetu hizi za leo.

23-Na wanaadhini kama wanavyoadhini Waislamu wengine isipokuwa ni kwamba wao baada ya ibara: 'Hayya alal-falaa' –huweka jumla isemayo 'hayya alaa khairil-amal' kwa sababu ibara hiyo ilikuwepo katika adhana katika zama za Mtume wa Mwenyezi Mungu. Kwa hakika aliifuta- kwa ijtihadi yake-mwenyewe Omar binil-Khattab kwa hoja kwamba iliwaondoa na kuwafanya Waislamu wasiielekee kwenye jihadi, ikiwa watafahamu kuwa swala ndiyo amali iliyo bora (kama alivyosema wazi kuhusu hilo Allamah Qawshajiy al-Ssh'ariy katika kitabu chake Sharhut-Tajriidil-Iitikadi, na imekuja katika kitabu al-Muswannif cha al-Kindiy na Kanzul-Ummal cha al-Muttaqiy al-Hindi na wengineo). Wakati huohuo Omar binil-Khattab aliongeza ibara isemayo 'As-swalatu Khairu minan-Nawmi', wakati ambapo ibara hiyo haikuwamo kwenye adhana katika zama za Mtume (SAW). (Rejea vitabu vya hadithi na historia).

Kutokana na ukweli kwamba ibada na vitangulizi vyake katika Uislamu vinategemea amri takasifu ya kisheria na idhini yake, kwa maana kwamba ni wajibu kila kitu kijitegemeze kwenye dalili ya wazi (Nassi) maalumu au ya ujumla kutoka kwenye Kitabu na Sunna, la sivyo itakuwa ni bid'ah (uzushi) inayopaswa kupingwa na kurejeshwa kwa mwenye kuizusha,

kwa hivyo haiwezekani kuzidisha au kupunguza jambo lolote lile katika ibada, bali katika mambo mengine yote ya kisheria kwa kufuata rai na maoni ya mtu binafsi.

Ama wayaongezayo Mashia Jaafariyyah baada ya ibara

أَشْهَدُ أَنَّ مُحَمَّداً رَسُولُ اللهِ

pindi wasemapo

أَشْهَدُ أَنَّ عَلِيّاً وَلِيُّ اللهِ

hilo imetokana na riwaya zilizopokelewa kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu na Ahlul-Bait wake, rehma za Allah ziwe juu yao, zisemazo wazi kuwa haitajwi jumla isemayo 'Muhammad Rasuulullah' au kuandikwa juu ya mlango wa pepo isipokuwa hufuatiwa na jumla isemayo:

عَلِيٌّ وَلِيُّ اللهِ

Na hiyo ni jumla itoayo habari kuwa Mashia hawasemi kuwa Ali (AS) ni mtume, seuze kusema kuwa ni Mungu na Mola. Tunajikinga na Mwenyezi Mungu kutokana na kauli hizo.

Kwa sababu hiyo ndio maana ikajuzu kuitaja pembezoni mwa shahada mbili kwa kutaraji kuwa iwe ni yenye kutakiwa na ni jambo jema mbele ya Mwenyezi Mungu mtukufu. Haitamkwi ibara hiyo wala kuletwa kwenye adhana kwa kukusudia kuwa ni sehemu ya adhana au kuwa ni wajibu na hii ndiyo kauli inayofuatwa na maulama wengi wa Shia Jaafariyyah.

Kutokana na haya, hakika kuzidisha huku kufanywako bila kukusudia kuwa ni sehemu ya adhana kama tulivyosema, hakuhesabiwi kama ni jambo lisilokuwa na asili katika sheria, na kwa hivyo haiwi ni bid'ah.

24- Wanasujudu juu ya udongo (na mchanga) au juu ya vijiwe (changarawe), au juu ya jiwe kubwa na vinginevyo kati ya sehemu za ardhi na mimea yake (kama kuti) na si zulia na kitambaa na vitu vyenye kuliwa na mapambo,

kutokana na riwaya nyingi zilizopokelewa katika vitabu vya Kishia na Kisunni ya kwamba Mtume (SAW) alikuwa na kawaida ya kusujudu juu ya udongo au juu ya ardhi, bali aliwaamuru Waislamu kufanya hivyo. Miongoni mwa mifano ya hilo ni kwamba Bilal siku moja alisujudu juu ya pindo la kilemba chake kwa ajili ya kujikinga na joto kali lenye kuunguza, Mtume akaondoa kilemba kile kwa mkono wake kutoka kwenye paji lake la uso na kusema: 'Ewe Bilal! Weka paji lako la uso juu ya udongo.'
Na pia aliyasema maneno kama haya kwa Suhaibu na Rabah, pindi aliposema: 'Ewe Suhaib! Weka uso wako juu ya udongo na ewe Rubah! Weka uso wako juu ya udongo.' (Rejea al-Bukhari, na Kanzul-Ummal, na al-Muswannif cha Abdur-Razzaq as-San'aaniy, na as-Sujuudu alal-ardhi cha Kaashiful-ghitaa).

Na kwamba Mtume (SAW) alisema-kama ilivyonukuliwa katika Sahihi Bukhari na katika vitabu vinginevyo:-

جُعِلَتْ لِيَ الأَرْضُ مَسْجِداً وَطَهُوراً.

'Nimejaaliwa (nimefanyiwa) ardhi kuwa mahala pa kusujudia na kujitwahirishia.'
Na kutokana na ukweli kwamba kusujudu juu ya udongo na kuweka paji la uso wakati wa kusujudu juu ya ardhi ndio sehemu inayofaa zaidi kwa ajili ya kumsujudia Mwenyezi Mungu, kwani hilo ndilo limpelekealo zaidi mja kwenye unyenyekevu na hilo ndio lililo karibu zaidi na khudhuui mbele ya mwenye kuabudiwa, kama ambavyo kusujudu juu ya ardhi kunamkumbusha mwanadamu asili yake na madini aliyoumbiwa. Je, si Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

ﭽ ﭼ ﭽ ﭼ ﭽ ﭼ ﭽ ﭼ ﭽ

(Kutokana na udongo huo tumekuumbeni na tutakurudisheni kwenye udongo na humo tutakutoeni kwa mara nyingine tena)?.[1]

Na kwamba kusujudu ndio mwisho na daraja la juu zaidi la unyenyekevu, na kikomo cha khudhuui hakithibiti kwa kusujudu juu ya mswala na farshi, na kitambaa na johari zenye thamani, bali kunathibiti kwa kuweka sehemu tukufu sana mwilini ambayo ni paji la uso juu ya kitu rahisi sana ambacho ni udongo. (Rejea: al-Yawaaqiit wal-Jawaahir cha Shaaraniy al-Answariy al-Misriy kati ya wanazuoni wa karne ya kumi).
Naam, udongo unapasa kuwa msafi na ndio maana Mashia wakawa wanabeba, kipande cha udongo (nao ni udongo ulio finyangwa pamoja) ili kuwa na uhakika na kuthibitisha utwahara (usafi) wake. Na huenda udongo huu ukawa umechukuliwa kwenye ardhi yenye baraka kama vile ardhi ya Karbalaa ambapo Alifia shahidi kwenye ardhi hiyo Imam Husein (AS) Mjukuu wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (SAW) kwa ajili ya kutabaruku, kama baadhi ya maswahaba walivyokuwa wakichukua changarawe za Makka kwa ajili ya kusujudu juu yake wakiwa safarini, kwa ajili ya kutabarruk (Rejea: al-Muswannif cha Swan'aaniy).
Lakini Mashia Jaafariyyah hawang'ang'anii juu ya jambo hili, na wala hawajilazimishi kulifanya hilo wakati wote, bali husujudu juu ya jiwe lolote lililo safi kama vile marumaru zilizotandikwa kwenye msikiti wa Mtume mtukufu (SAW), na marumaru za Masjidul-Haraam bila ya kuwa na ishkali yoyote wala kutatizika.

[1]-Suurat Twaha aya 55.

Wao hawaweki mkono wao wa kulia juu ya mkono wa kushoto katika swala, kwa sababu Mtume (SAW) hakufanya hivyo, na kutokana na ukweli kuwa halikuthibiti hilo kwa dalili ya wazi iliyo thabiti na isiyo na shaka, kutokana na sababu hii ndio maana wafuasi wa Maaliki hawalifanyi hilo pia (Rejea: al-Bukhariy na Muslim na Sunanul-Baihaqiy, na kwa ajili ya kuelewa rai ya Maaliki rejea kwenye kitabu Bidayatul-Mujtahid cha Ibnu Rushdi al-Qurtubiy al-Maalikiy na vinginevyo).

25- Shia Jaafairayyah wanatawadha kwa kuosha mikono yao kuanzia kwenye kiwiko hadi kwenye ncha za vidole na si kinyume chake, kwa sababu wao walichukua udhu na namna ya kutawadha kutoka kwa Maimamu wa Ahlul-Bait (AS) ambao nao waliuchukua kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (SAW). Wao ndio wanaoelewa zaidi kuliko watu wengine alivyokuwa akifanya babu yao yaani Mtume (SAW) kuhusiana na suala hili. Walilifasiri neno 'Ilaa' lililoko kwenye aya inayoelezea udhu [1] kwa maana ya 'Ma'a' (pamoja), kama alivyofanya Shaafii' as-Swaghiir katika kitabu chake: (Nihayatul-Muhtaaj).
Kama ambavyo wao hupaka miguu yao na vichwa vyao na wala hawaoshi katika udhuu kutokana na sababu hiyo hiyo ambayo tumeitaja, na pia kwa sababu Ibnu Abbas amesema: "Udhu una sehemu mbili za kuosha na sehemu mbili za kupaka, au mahala pawili pa kuosha na mahala pawili pa kupaka.' (Rejea Sunan na al-Masaaniid, na pia rejea Tafsiir Fakhrur-Raziy katika kuifasiri aya ya udhu).

[1]-Suuratul-Maaidah aya 6.

26- Na wanasema ya kuwa inajuzu kuoa ndoa ya muta'a kutokana na dalili ya Qur'an Tukufu kuruhusu kufanya hivyo pale iliposema:

ڤ ڤ ڤ ڤ ڤ ڤ

(Na mtakapostarehe nao basi wapeni malipo yao).[1]

Na kwa sababu ilifanywa na Waislamu katika zama za Mtume wa Mwenyezi Mungu na masahaba zake kuitekeleza hadi katika nusu ya utawala na ukhalifa wa Omar binil-Khattab, nayo ni ndoa ya kisheria inayoshirikiana na ndoa ya daima katika mambo kadhaa:

a. Mwanamke asiwe ameolewa au mwenye mume, kusoma swigha ya ndoa yenye sehemu mbili 'iijabu' kutoka kwa mwanamke na 'kabuul' (kukubali) kutoka kwa mwanamume.
b. Katika wajibu wa kumpa mwanamke malipo katika ndoa ya daima huitwa kwa jina la mahari, na katika ndoa ya muta'a huitwa al-ajri (malipo au ujira), kutokana na nassi na dalili ya wazi ya Qur'an kama tulivyonukuu hapo juu kwenye aya.
c. Katika wajibu wa kukaa eda mwanamke baada ya kutengana kati ya mume na mke.
d. Katika wajibu wa kukaa eda baada ya kufarakana, na mtoto kuambatanishwa na kumfuata mzazi wa kiume, na wajibu wa mume kuwa mmoja na si zaidi.
e. Katika kurithiana kati ya mtoto na baba, na mtoto na mama na kinyume chake pia.

Na inatofautiana na ndoa ya daima katika suala la kubainisha muda katika ndoa ya muta'a na kutokuwa wajibu kutoa

[1]-Suratun-Nisaai aya 24.

matumizi na mume kugawa masiku kwa mke, na kutorithiana kati ya mume na mke, na kutokuwa na haja ya kutalikiana kwa ajili ya kutengana, bali inatosha kumaliza muda au kusamehe sehemu ya muda uliotajwa katika nasi ya mkataba na akdi ya ndoa.

Na hekima ya kuwekwa ndoa ya aina hii kisheria ni kwa ajili ya kuitika na kujibu mahitaji ya kisheria na yaliyoshurutishwa na mahitaji ya kijinsia ya mwanaume na wanawake na kwa yule asiyeweza kutekeleza mambo yote yanayomlazimu mtu anayetaka kufunga ndoa ya daima, au aliye zuiliwa kuoa, kutokana na kifo au sababu nyingine na kinyume chake, pamoja na kuwa na nia ya kuishi maisha mema na yenye sharafu. Kwa hivyo basi, Muta'a katika daraja la kwanza ni utatuzi wa matatizo muhimu ya kijamii, na ni kwa ajili ya kuzuia jamii ya Kiislamu kutumbukia kwenye janga la ufisadi na uhalalishaji wa mambo ya haramu.

Na yawezekana kufaidika kutokana na ndoa hiyo na kutumika kwa ajili ya malengo ya kuelewana na urafiki wa kisheria kabla ya kuoana kupitia ndoa ya daima. Kwa hivyo ndoa hiyo ni njia nzuri ya kuzuia kufanya mambo ya haramu kama vile zinaa, na ukinzani wa kijinsia au kutumia mambo mengine yaliyoharamishwa kama vile kupiga punyeto kwa yule asiyeweza kuvumilia kukaa na mke mmoja, au hawezi kumuendesha na kukaa na mke mmoja- au zaidi ya mke mmoja- kiuchumi na kimaisha na wakati huohuo hataki kufanya matendo ya haramu.

Ala kulli haal, hakika ndoa hii inajitegemeza kwenye Kitabu na Sunna, na maswahaba waliitekeleza katika kipindi fulani,

na lau kama ingekuwa ni zinaa ingekuwa na maana ya kuwa Qur'an na Mtume na maswahaba wamehalalisha zinaa na mwenye kuifanya muta'a atakuwa amefanya zinaa kwa kipindi fulani cha umri wake! Tunajikinga na Mwenyezi Mungu na hilo.

Hii ni mbali na kuwa kufutwa kwake hakukutegemezwa kwenye Kitabu na Sunna, na wala hakuna dalili iliyo thabiti na ya wazi ithibitishayo hilo.[1]

Mashia Imamiyyah pamoja na kuwa wanahalalisha na kuiruhusu ndoa ya aina hii iliyowekwa na sheria na iliyoruhusiwa kwa nassi na dalili za Kitabu na Sunna lakini ukweli ni kuwa wanapendeelea zaidi ndoa ya daiama na kuunda familia kutokana na kwamba famili ndio msingi wa jamii yenye nguvu na iliyo salama, na wala hawapendelei na kumili kwenye kufunga ndoa ya muda inayoitwa katika sheria kwa jina la muta'a pamoja na kuwa ndoa hiyo- kama tulivyosema- ni ndoa halali na iliyoruhusiwa kisheria.

Kwa taarifa ya msomaji ni kwamba, hakika Mashia Imamyyah- kutokana na Kitabu na Sunna na mafunzo na usia mbali mbali za Maimamu wa Ahlul-Bait (AS)- humuonyesha mwanamke heshima na kumpa hadhi kubwa. Wana sheria nzuri, za kuvutia na zinazopaswa kuzingatiwa katika riwaya za Maimamu na vitabu vyao vya fiqhi kuhusiana na suala la nafasi na haki za mwanamke na hasa katika uwanja wa kuamiliana naye kitabia na kimaadili na katika mambo ya umiliki, ndoa, talaka, kulea watoto, kunyonyesha, ibada na miamala mingine mbali mbali.

---

[1]-Rejea hadithi zote zielezeazo ndoa ya muta'aa katika vitabu Sahihi na Masaaniid na Sunan vyenye kuzingatiwa na madhehebu tofauti za Kiislamu.

27- Na Shia Jaafariyyah: wanaharamisha zinaa, kulawiti, kula riba, kuua nafsi iliyo haramishwa kuuliwa bila sababu, kunywa pombe, kamari, kufanya vitimbi na hila, hadaa na udanganyifu (ghushi), kulimbikiza chakula kwa ajili ya kukiuza kwa bei kubwa, kupunguza vipimo au mizani, unyang'anyi, wizi, kufanya khiyana, miziki na kucheza, kumtuhumu mtu kwa uzinifu, tuhuma, uchochezi na ufisadi, kuwaaudhi waumini, kusengenya, kutukana na kusema maneno machafu, kusema uongo na kuzua na mengineyo yasiyo kuwa hayo kati ya madhambi makubwa na madogo. Hujaribu- wakati wote -kujiepusha na mambo hayo, na kutoyatenda vyovyote iwezekanavyo.
Na wanafanya juhudi za kuyazuia yasitokee katika jamii kwa njia tofauti kama vile kutunga, kuandika na kusambaza vitabu na majarida ya kimaadili na kimalezi, kufanya vikao na mihadhara, na kupitia khutuba za ijumaa n.k.

28- Na wanatilia umuhimu maadili na tabia bora na tukufu, na wanapendelea sana mawaidha, na huharakia kusikiliza mawaidha hayo, na kwa ajili hiyo hufanya majlisi na vikao kadhaa majumbani na misikitini na sehemu za wazi, katika minasaba na misimu mbali mbali kutokana na kupenda kwao kusikiliza mawaidha na kuwaidhika. Kutokana na haya hutilia umuhimu sana dua tukufu na nzuri na zenye faida, zenye madhumuni makubwa zilizopokelewa kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (SAW) na Maimamu watwaharifu watokanao na Ahlil-Baiti wake kama vile: Duau Kumaili, Duau Abi Hamzah at-Thamaliy, Duau Samaat,

Duau Jawshanil-Kabiir[1], Duau Makaarimul-Akhlaaq, na Duaul-Iftitah (ambayo husomwa katika mwezi wa Ramadhani). Wao husoma dua hizi na munajaati (nong'ono) hizi zenye madhumuni ya hali ya juu kwa unyenyekevu wa kiroho, na wakiwa katika hali ya kulia na kunyenyekea kwa Mwenyezi Mungu, kwa sababu dua hizo huzilea na kuzihadhibisha nafsi zao na kuwakaribisha kwa Mwenyezi Mungu. (Dua hizi zipo kwenye mjumuiko wa dua uitwao Mawsuuatul-Ad'iyatil-Jaamiah ulioandikwa hivi mwishoni, na pia kwenye vitabu vyao vingine mashuhuri vya dua).

29-Na wao hutilia umuhimu sana makaburi na marqad ya Mtume na Aali zake (sehemu alipozikiwa), na maraaqid za Maimamu wa Ahlil-Baiti watwahaarifu waliozikwa katika uwanja wa Bakii'i, yaliyoko katika mji wa Madinatul-Munawarah sehemu yalipo makaburi ya Imam Hasan Mujtaba, Imam Zainul-Aabidiin, Imam Muhammad al-Baaqir, na Imam Jaafar as-Swaadiq (AS).

Na katika mji mtukufu wa Najaf mahala ambapo kuna kaburi la Imam Ali (AS). Na katika mji wa Karbalaa mahala ambapo kuna kaburi la Hussein bin Ali (AS) na ndugu zake na watoto wake na watoto wa ami zake, na maswahaba wake ambao walikufa mashahidi pamoja naye siku ya Ashuraa.
Na katika mji wa Samarra mahali ambapo kuna kaburi la Imam al-Hadiy na Imam Askariy (AS).

[1]-Hii ni dua iliyokusanya majina elfu moja kati ya majina ya Allah yaliyo pangiliwa katika mpango mzuri na wa kuvutia.

Na katika mji wa Kaadhimiyyah mahala ambapo kuna Makaburi ya Maimamu wawili Imam al-Jawaad na Imam Kaadhim (AS). Miji yote hiyo iko katika nchi ya Iraq.
Na katika mji wa Mash'had ulioko Iran mahala ambapo kuna kaburi la Imam Ridhaa (AS).
Na katika mji wa Qum, na Shiraz mahala ambapo kuna makaburi ya watoto wao na mabinti zao, na katika mji wa Damascus mahala ambapo kuna kaburi la shujaa wa Karbalaa Sayyidatu Zainab.
Na katika mji wa Cairo mahala ambapo kuna kaburi la Sayyidah Nafiisah (huyu ni miongoni mwa mabibi watukufu wa Ahlil-Baiti).
Na hufanya hivyo kwa ajili ya heshima ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (SAW), kwa sababu mtu huhifadhiwa katika kizazi chake, na kuwakirimu kizazi cha mtu ni sawa na kumkirimu mtu huyo. Na pia kwa sababu Qur'an Tukufu iliwasifu Aali Imraan, na Aali Yaasin na Aali Ibrahiim na Aali Yaakub na kuwatukuza, hali ya kuwa baadhi yao hawakuwa mitume, kwa kusema:

ﮒ ﮓ ﮔ ﮕ
(Ni kizazi cha wao kwa wao).[1]

Na kwa sababu Qur'an haikuwakemea wale waliosema:

ﮊ ﮋ ﮌ
Bila shaka sisi tutajenga msikiti juu yao.[2]

Yaani hakika tutajenga na tutasimamisha msikiti juu ya makaburi ya As'haabul-Kahf, ili aabudiwe Mwenyezi Mungu pembezoni mwao, na hakuisifu kazi yao na kuielezea kuwa ni shiriki, kwa sababu Muislamu muumini anarukuu na kusujudu kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na anamuabudu yeye peke yake. Kwa hakika hufanya hivyo pembezoni mwa kaburi au Dharihi la mawalii watwaharifu kutokana na mahala hapo kupata utukufu kutokana na wao kulazwa hapo, kama ilivyofanyika kwenye Maqaamu Ibrahiim kwani sehemu hiyo ilipata utukufu na karama na Mwenyezi Mungu mtukufu akasema:

ﮋ ﮊ ﮉ ﮈ
(Na wakaifanya (Maqaamu Ibraahim) sehemu aliyosimama Ibrahiim kuwa ni sehemu ya kuswalia).[3]
Na mwenye kuswali nyuma ya Maqaamu Ibrahiim hawi ni mwenye kuabudu Maqaamu, na wala mwenye kumuabudu Mwenyezi Mungu kwa kufanya Saai kati ya Swafa na Marwa atakuwa ameabudu vijilima hivyo viwili. Hakika Mwenyezi Mungu amewachagulia waja wake mahala patakatifu pa

[1]-Suuratu Aali Imran aya 34.
[2]-.Suuratul-Kahfu aya 21.
[3]-Suuratul-Baqarah aya 125.

kumuabudia Yeye kutokana na mahala hapo kuhusiana Naye kwa njia moja au nyingine. Ni wazi kuwa masiku na mahala tofauti pana utukufu maalumu, kwa mfano siku ya Arafa na ardhi ya Mina na pia Arafa. Siku na sehemu hizo zina utukufu maalumu kutokana na kunasibishwa kwao kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu.

30- Na kwa sababu hii pia, Shia Jaafariyyah hutilia umuhimu-kama Waislamu wengineo wenye ufahamu na wenye kuelewa utukufu wa Mtume wa Mwenyezi Mungu na Ahlul-Bait wake watwaharifu- kuzuru makaburi ya Ahlul-Bait (AS), kwa ajili ya kuwakirimu, kuchukua mazingatio kutoka kwao, kujadidi ahadi pamoja nao, kusisitiza juu ya malengo ya hali ya juu ambayo walipigana jihadi kwa ajili yake na wakafa mashahidi kwa ajili ya kuyalinda na kuyahifadhi. Watu wanaozuru makaburi haya hutaja katika ziara hizo fadhila za wenye makaburi hayo, jihadi yao, kusimamisha kwao swala, kutoa kwao zaka na kuendeleza waliyoyavumilia katika njia hiyo kati ya maudhi na mateso, ukiongezea kule kushirikiana na Mtume Mkarimu- kwa kuwafanyia upole kizazi chake kilichodhulumiwa- kutokana na huzuni yake (SAW) kwao.

Je, si ni yeye aliyesema kuhusiana na tukio la kufa shahidi Hamzah:

لَكِنَّ حَمْزَةَ لاَ بَوَاكِيَ لَهُ!

'Lakii Hamzah hana watu wa kumlilia'. (kama ilivyoelezwa katika vitabu vya historia na sira)?

Je, si ni yeye aliyelia kutokana na kifo cha Ibraahim mwanawe mpenzi?

Na je, si ni yeye aliyekuwa akitoka na kwenda kuzuru makaburi ya Baqii'ai?

Je, si ni yeye aliyesema:

زُورُوا الْقُبُورَ فَإِنَّهَا تُذَكِّرُكُمْ بِالآخِرَةِ.

'Yazuruni makaburi kwa hakika yanakukumbusheni Akhera'? [1]

Ndio, hakika kuzuru makaburi ya Maimamu wa Ahlul-Bait wa Mtume na yasemwayo na kukumbukwa kati ya sera zao na misimamo yao ya kijihadi huvikumbusha vizazi vijavyo mambo na mchango walioutoa watukufu hao katika njia ya Uislamu na Waislamu kati ya ujitoleaji muhanga wa kishujaa, kama ambavyo hupandikiza katika nyoyo zao roho ya ushujaa na ushupavu na kujitolea muhanga na kufa shahidi katika njia ya Mwenyezi Mungu.

Kwa hakika kufanya hivyo ni kitendo na kazi ya kiutu na kiutamaduni na ya kiakili. Kwa mfano, tunaona umma mbali mbali zikihifadhi milele watukufu na viongozi wao wakubwa, na waanzilishi wa utamaduni wa umma hizo na kuhuisha minasaba yao kwa aina na namna mbalimbali. Hii ni kwa sababu kufanya hivyo hupelekea kupata fakhari na utukufu (izza) mambo yao waliyoyafanya na kuyatekeleza. Jambo hilo pia huzipa umma hizo kuendelea kushikamana na mambo hayo waliyoyafanya na kushikamana na madili yao.

Na haya ndiyo yele yale yaliyokusudiwa na kutakiwa na Qur'an pindi iliposifia na kuelezea katika aya zake misimamo ya mitume na mawalii wema na kutaja visa vyao.

31- Na Shia Jaafariyyah huomba shaafaa kupitia kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (SAW) na Maimamu watwaharifu wa

[1]-Shifaus-Siqaam cha as-Sabkiy Shafi'i ukurasa 107, na hadithi nyingine kama hiyo iko kwenye Sunanu Ibnu Maajah juzuu 1 \ 117.

Ahlul-Bait (AS) na wanatawasali kwa Mwenyezi Mungu kupitia kwao, kwa ajili ya kughufiriwa madhambi, kukidhiwa haja na kwa ajili ya kutibu wagonjwa, kwani Qur'an ndiyo ambayo iliruhusu kufanya hivyo bali iliwahimiza na kuwataka watu kufanya hivyo, kama inavyosema:

ۀ ھ ھ ے ے ۓ ۓ ڭ ڭ ڭ ڭ ۇ ۇ ۆ ۆ ۈ

'Na lau wangelikuja walipojidhulumu nafsi zao wakaomba msamaha kwa Mwenyezi Mungu, na (yeye) Mtume pia akawaombea msamaha bila shaka wangemkuta Mwenyezi Mungu ni mwingi wa kukubali toba na mwenye kurehemu'.[1]

Na amesema:

(Na Mola wako atakupa na utaridhia).[2]

na hicho ni cheo cha uombezi.

Vipi inaingia akilini Mwenyezi Mungu ampe Mtume wake mtukufu cheo cha kuwaombea watu wenye madhambi, na cheo cha wasila kwa ajili ya watu wenye haja na matatizo kisha awazuwie watu hao kuomba shafaa kutoka kwake, au amuharamishie Mtume kutumia cheo hicho?!

Je, si Mwenyezi Mungu anasimulia habari za watoto wa Yaakub ya kwamba wao waliomba uombezi na shafaa kutoka kwa baba yao kwa kusema:

ڈ ڈ ڤ ڤ ڤ ڤ ڤ ڤ

'Ewe baba yetu! Tuombee msamaha kwa dhambi zetu, hakika sisi tulikuwa ni wenye kufanya makosa'.[3]

[1]- Suuratun-Nisaa aya 64.
[2]-Suuratu Dhuhaa aya 5.
[3]- Suuratu Yuusuf aya 97-98.

Na Mtume mtukufu na ambaye ni maasumu hakuwakataza kusema hivyo bali aliwaambia:

ڤ ڤ ڄ ڄ ڄ

'Nitawaombea msamaha' [1]

Na haiwezekani kwa mtu yeyote kudai kwamba Mtume na Maimamu (rehma za Mwenyezi Mungu ziwe juu yao) wamekufa, na kwa hiyo kuomba dua kutoka kwao hakuna faida yoyote. Hilo ni kutokana na ukweli kwamba, mitume na hasa Mtume wa Mwenyezi Mungu (SAW) wako hai. Mwenyezi Mungu amesema kuhusiana na Mtume huyo Mtukufu (SAW):

ڤ ڤ ڤ ڤ ڤ ڤ ڄ ڄ ڄ ڄ

(Na hivyo hivyo tumekufanyeni Umma bora ili muwe mashahidi juu ya watu, na Mtume awe shahidi juu yenu)[2]

Yaani awe ni mwenye kushuhudia.

Na amesema:

ڤ ڤ ڤ ڤ ڤ ڤ ڤ

'Na sema: Fanyeni matendo (mema). Mwenyezi Mungu atayaona matendo yenu hayo na Mtume wake na waumini'.[3]

Aya hii ni yenye kuendelea na kutumika hadi Siku ya Kiyama madamu jua na mwezi ni vyenye kufanya kazi, na kuendelea kuwepo kwa usiku na mchana.

Na pia ni kutokana na ukweli kwamba Mtume na Maimamu watokanao na Ahlul-Bait wake ni mashahidi, na mashahidi wako hai, kama alivyosema Mwenyezi Mungu Mtukufu zaidi ya mara moja katika Kitabu chake kitukufu.

[1]-Suuratu Yusuf aya 97-98.
[2]-Suuratul-Baqarah aya 143.
[3]-Suuratut-Tawbah aya 105.

32-Na Shia Jaafariyyah husherehekea kuzaliwa kwa Mtume na Maimamu watokanao na Ahlul-Baiuti wake (AS), na kuomboleza katika siku za kufariki kwao. Hukumbuka kwenye maombolezo hayo fadhila, sifa zao njema na misimamo yao mizuri, ambayo imepokelewa kwa njia sahihi kutokana na Qur'an tukufu ambayo imetaja sifa za Mtume (SAW) na mitume wengine. Imewasifu na kuwasihi watu kuwazingatia kwa makini watukufu hao kwa ajili ya kuwafuata na kuwafanya kuwa vigezo na viongozi wao.

Naam, Shia Jaafariyyah hujitenga na kujiepusha na vitendo vilivyoharamishwa katika majlisi hizo, kama vile kuchanganyika kulikoharamishwa kati ya wanawake na wanaume na kula vyakula vilivyoharamishwa na vinywaji pia. Hujiepusha pia kuvuka mipaka katika kusifu,[1] na matendo mengine ambayo yanapingana na sheria takasifu ya Kiislamu, isiyo na shaka kuhusiana na usahihi wake kwa msingi wa Qur'ani Tukufu na Sunna za Mtume (SAW).

33- Na Shia Jaafariyyah wanatumia vitabu vyenye hadithi za Mtume Mtukufu na Ahlul-Bait wake watwaharifu (SA). Kwa mfano, kitabu al-Kaafii cha Thiqatul-Islaam al-Kulainiy, Man Laa Yahdhuruhul-Faqiihu cha Shekh

[1]-Na Ghuluwwi (kuvuka mipaka katika kusifu) ni kumuinua mtu daraja lake hadi kufikia kwenye cheo cha uungu, au kuitakidi ya kuwa mtu huyo anafanya mambo yeye mwenye akiwa mustakilli bila kumtegemea Mwenyezi Mungu na bila ya kuutegemea utashi wa Mwenyezi Mungu na idhini yake, kama wafanyavyo Wakiristo na Mayahudi kuhusiana na mitume na manabii wao.

Swaduuq, al-Istibswaar na Tahdhiib cha Shekh Tuusiy. Hivyo ni vitabu madhubuti katika nyanja za hadithi.
Vitabu hivi, japokuwa vimekusanya hadithi sahihi ila ukweli ni kuwa si waandishi wala Mashia Jaafariyah wamevitaja kuwa ni 'Sahihi.' Kwa sababu hii, wanazuoni wa fiqhi wa Kishia hawasemi kuwa hadithi zote zilizomo kwenye vitabu hivyo ni sahihi, bali huchukua zile zilizo thibiti kwao kati ya hadithi hizo, na kuziacha zile wazionazo kuwa si sahihi kulingana na kanuni za elimu ya hadithi.

34- Kama ambavyo – katika nyanja za itikadi, fiqhi, dua na Akhlaq- hutumia vitabu vingine ambavyo ndani yake kulipokelewa riwaya za aina tofauti kutoka kwa Maimamu watwaharifu kama vile kitabu kiitwacho: 'Nahjul-Balagha' ambacho kimetungwa na Sayyid Radhiy (Mungu amrehemu) kinachojumuisha: Khutuba, barua na jumla fupi za hekima za Imam Ali (AS).
Vitabu vingine ni kama vile Risaalatul-Huquuq na Swahifatus-Sajjadiyyah vya Imam Zainul-Aabidiin Ali bin Husein (AS), Swahifatul-Alawiyyah cha Imam Ali (AS), Uyuunul-Akhbaarir-Ridhaa, at-Tawhiid, al-Khiswaal, Ilalush-Sharaa'ii na Maanil-Akhbar cha Shekh Swaduuq (RA).

35- Wakati mwingine Mashia Jaafariyyah hutumia hadithi sahihi za Mtume (SAW) zilizopokelewa kwenye vyanzo vya ndugu zao wa Ahli Sunna wal-Jamaa'ah,[1] katika maudhui

[1]-Ni vyema kuashiria hapa ya kwamba, Shia Imamiyyah ndio Ahli sunna pia kwa sababu wao huchukua yaliyokuja kwenye Sunna ya Mtume iwe kauli matendo au kukiri kwake, na kati ya sunna hizo ni usia wa Mtume (SAW) kuhusu haki ya Ahlil-Baiti wake na hushikamana na usia huo kimatendo na kwa umadhubuti na itikadi,

tofauti bila ya kufanya taasubi au kuzidharau, na vitabu vyao vya zamani na vya sasa vinashuhudia juu ya hilo. Kwani zimepokelewa ndani yake hadithi kutoka kwa maswahaba wa Mtume (SAW), wake zake na maswahaba mashuhuri na wapokezi wakubwa wa hadithi kama vile Abi Hureirah na Anas na wengineo, kwa sharti kuwa ziwe sahihi, zisipingane na Qur'an na hadithi nyinginezo sahihi, akili salama na ijmai ya maulama.

36- Na Shia Jaafariyyah wanaona kwamba, matatizo, mitihani na mabalaa yaliyowapata Waislamu huko nyuma na yawapatayo hivi sasa hayatokei ila kutokana na mambo mawili yafuatavyo:
1-Kujighafilisha na kujifanya hawawatambui Ahlul-Bait (AS) kama viongozi wenye uwezo wa kuongoza, na kujitenga na maelekezo na mafundisho yao, na hasa tafsiri yao ya Qur'an Tukufu.
2-Kutengana, kuparaganyika, kuhitilafiana na kuzozana kati ya madhehebu na makundi mbalimbali ya Kiislamu.
Ni kutokana na sababu hii ndio maana Mashia Jaafariyyah wakafanya juhudi kubwa za kuunganisha safu za Umma wa Kislaamu, na huwanyooshea watu wote mkono wa mapenzi na udugu, wakiziheshimu ijtihadi za maulama wa madhehebu hizo na makundi hayo pamoja na kuziheshimu hukumu zao za kifighi.

---

fiqhi na vitabu vyao vya hadithi ni ushahidi bora na mzuri juu ya hayo. Hivi karibuni kimechapishwa kitabu kikubwa chenye jina la Mawsuuah Mufaswallah chenye juzuu kumi kilichokusanya riwaya za Mtume Mtukufu zilizomo kwenye vyanzo vya Kishia ziitwazo kwa jina la (Sunanun-Nabii).

Na katika njia hii, ni kawaida kwa Maulama wa Shia Jaafariyyah tangu karne za mwanzo za Kiislamu kutaja rai za mafaqihi wasio Mashia katika vitabu vyao vya kifiqhi, tafsiri na il-mul-kalaam (itikadi) kama vile: al-Khilaaf kinachohusu fiqhi, cha Shekh Tuusiy, na Majmaul-Bayaan kinachohusu tafsiri cha Tuusiy, na ambacho kimesifiwa na maulama wakubwa wa Az'har.
Kingine ni kitabu Tajriidul-Iitikadi cha Nasrud-Dini Tuusiy kinachohusiana na itikadi, na ambacho kilifanyiwa sherhe na Alaaud-Din al-Kawshaji al-Ash'ariy.

37- Na maulama wakubwa wa Shia Jaafariyyah wanaona kwamba kuna ulazima wa kufanyika mazungumzo kati ya maulama wa madhehebu tofauti za Kiislamu katika nyanja za fiqhi, Itikadi, historia na kufahamiana katika mambo yanayowahusu Waislamu wa zama hizi, na kujiepusha kutupiana tuhuma, na kulitia anga sumu ya kutukanana ili kuwe na mazingira bora na yaliyo munasibu kwa ajili ya kuweka ukaribu wa kimantiki kati ya makundi mbalimbali ya Kislaamu. Jambo hili likitimia bila shaka litailinda jamii kubwa ya Kiislamu na kuiwezesha kukabiliana vilivyo na maadui wa Uislaamu na Waislamu ambao wakati wote hutafuta mwanya wa kutelekeza hujuma na njama zao hatari dhidi ya jamii nzima ya Kiislamu bila ya kupendelea na kuwahurumia baadhi yao.

Kwa msingi huo, Shia Jaafariyyah kamwe hawam-kufurishi yeyote kati ya Waislamu (Ahlul-Kibla) kwa vyovyote vile yatakavyokuwa madhehbu yake ya kifiqhi na muelekeo wake wa kiitikadi, isipokuwa kikundi kile ambacho Waislamu

wote wamekubaliana juu ya ukafiri wake. Hawaruhusu Waislamu wengine kufanyiwa uadui wala njama. Wanaheshimu ijtihadi za makundi na madhehebu za Kiislamu na wanasema kuwa matendo ya mwenye kuhama kutoka kwenye madhehebu yake na kujiunga na Ushia Jaafariyyah yanatosheleza na ni yenye kuangusha taklifu kwa mtu, ikiwa atakuwa ameyate-keleza mambo hayo kwa mujibu wa madhehebu yake ya zamani. Haya ni pamoja na taklifu kama vile swala funga hija, zaka, ndoa, talaka, kuuza na kununua (miamala ya kibiashara) na mengineyo. Kwa hivyo si wajibu juu yake kusoma upya nikahi au ndoa na talaka madamu atakuwa alitekeleza mambo hayo kwa mujibu wa sheria za madhehebu yake.

Wao huishi sehemu yoyote ile na ndugu zao Waislamu bila ya kuwa na wasiwasi wowote kama wanavyofanya kuhusiana na ndugu na jamaa zao wa kawaida.

Naam, hawakubaliani na madhehebu za kikoloni kama vile Ubahai, Ubabiyyah na Ukadiani, bali huyapinga na kuyapiga vita na kuharamisha kujiunga na madhehebu hizo.

Na kama Mashia - baadhi ya wakati na sio wakati wote - hufanya taqiyyah, ikiwa na maana ya kuficha matendo yao ya kimadhehebu na kiitikadi, na hilo likiwa ni jambo linaloruhusiwa kisheria kwa mujibu wa Qur'an Tukufu na kuchukuliwa kuwa jambo la kawaida miongoni mwa madhehebu za Kiislamu katika mazingira ya mapigano (mivutano) makali ya kimadhehebu, basi hufanya hivyo kutokana na moja kati ya sababu mbili:

1- Kuzilinda nafsi zao na damu zao ili zisimwagike ovyo.

2- Kuhifadhi na kulinda umoja wa Waislamu na kuuepusha mparaganyiko.

38- Na Shia Jaafariyyah wanaona kwamba miongoni mwa sababu za kubaki nyuma Waislamu hii leo, ni kuchelewa na kubaki kwao nyuma kifikra, kitamaduni, kielimu na kiteknolojia. Ufumbuzi wa tatizo hili ni kuwaelimisha Waislamu wanaume kwa wanawake, na kuinua kiwango chao cha kifikra, kitamaduni na kielimu kwa kuanzisha vituo vya kielimu kama vile vyuo vikuu pamoja na kufaidika na maendeleo ya kielimu ya kisasa katika kutatua matatizo ya kiuchumi, kiujenzi na kiviwanda. Jambo hilo pia linaweza kutimia kwa kuandaa mazingira ya kujiamini katika Umma wa Kiislamu ili kuupa msukumo wa kuingia kwenye nyanja za kazi na teknolojia na hivyo kuufanya kujitosheleza katika kila nyanja. Jambo hilo bila shaka litaufanya Umma kutokomeza hali ya kuwategemea wageni wa Magharibi katika kila jambo.

Na kwa sababu hii ndio maana Shia Jaafariyyah, popote walipo na waishipo wakaanzisha vituo vya kielimu na mafunzo, na kujenga vyuo kwa ajili ya kutayarisha na kuwaandaa wasomi na wataalamu walio na ujuzi mkubwa katika elimu tofauti. Kama walivyoingia kwenye vyuo vikuu na vyuo vya kawaida katika nchi mbali mbali, na kuhitimu maulama na wanazuo wenye ujuzi katika nyanja tofauti za kimaisha.

39- Shia Jaafariyyah huwasiliana na maulama na mafuqahaa wao kupitia njia ijulikanayo miongoni mwao kama taqliid katika sheria. Hurejea kwa maulama hao katika matatizo yao ya kifiqhi na katika nyanja zote za maisha yao. Hutekeleza matendo yao kwa mujibu wa rai za mafaqihi wao, kwa

sababu mafuqahau, kwa mujibu wa imani yao, ni mawakili na wawakilishi wa Imam wa Mwisho kati ya maimamu watwaharifu na ni manaibu wake. Kutokana na ukweli kwamba maulama na mafuqaha wao hawahitajii serikali wala watawala wa dola katika kuwapa fedha za kukidhia mahitaji yao maishani, ndio maana wakawa ni wenye kuaminika na kutegemewa sana na wafuasi wa madhehebu hii muhimu.
Hawzah za elimu za kidini- hivi ni vituo vya kulea mafuqahaa- ndizo huwatekelezea na kukidhi mahitaji yao ya kiuchumi kutokana na mali ya khumsi na zaka ambazo hutolewa na wafuasi wa madhehbu hii kwa utashi wao na kwa kutii amri ya Allah. Huitoa kama sehemu ya wadhifa wa kisheria kama vile watekelezavyo swala na funga.
Kuhusiana na wajibu wa kutoa khumsi kwa Mashia Imamiyyah ambayo hutokana na faida za kibiashara, kuna dalili nyingi na za wazi, na baadhi ya dalili hizo zimepokelewa katika vitabu kadhaa sahihi na Masaanid pia, (Rejea vitabu vyenye kuelezea (Mabahithul-Khumsil-Istidlaaliy Inda Fuqahau Shia).

40- Mashia Jaafariyyah wanasema kwamba ni haki ya Waislamu kuwa na serikali na tawala za Kiislamu ambazo zinapasa kutekeleza majukumu yao kwa mujibu wa Kitabu cha Allah na Sunna, zenye kulinda na kuhifadhi haki za Waislamu, kuwa na uahusiano wa kiadilifu na amani na madola mengine ya ulimwengu. Serikali kama hizo zinapasa kulinda mipaka yao na pia uhuru wa Waislamu kiutamaduni, kiuchumi na kisiasa, ili kuwaletea Waislamu izza na utukufu kama Mwenyezi Mungu alivyowataka wawe pale aliposema:

ﮓ ﮔ ﮕ ﮖ

(Na utukufu hasa ni wa Mwenyezi Mungu na Mtume wake na waumini).[1]
Pia amesema:

ﮘ ﮙ ﮚ ﮛ ﮜ ﮝ ﮞ ﮟ ﮠ ﮡ ﮢ

(Na wala msilegee wala msihuzunike, maana nyinyi ndio mtakaokuwa juu ikiwa mnaamini kweli).[2]
Na Mashia wanaamini kwamba Uislamu, kutokana na sifa yake kuwa ni dini iliyokamilika pande zote ina mfumo madhubuti wa utawala, na kwamba ni juu ya wanazuoni wa Umma huu mkubwa wa Kiislamu kukusanyika na kufanya mazungumzo kati yao ili kudhihirisha sura halisi ya mfumo huu wa utawala. Wanasema hilo litauwezesha Umma huu kujitoa kwenye utata na matatizo yasiyo na kikomo, na Mwenyezi Mungu ndiye mtoa ushindi na msaidizi.

ﮣ ﮤ ﮥ ﮦ ﮧ ﮨ ﮩ

(Ikiwa mtamnusuru Mwenyezi Mungu basi naye atakunusuruni na kukufanyeni muwe imara).
Hii ndiyo mifumo na misingi muhimu kuhusiana na itikadi na sheria za Mashia Imamiyyah ambo pia hujulikana kwa jina la Shia Jaafariyyah.

Na wafuasi wa madhehebu hii, hii leo wanaishi pembezoni mwa ndugu zao Waislamu katika nchi zote za Kiislamu. Madhehebu hii ina hamu kubwa ya kulinda na kuhifadhi Uislamu na Waislamu pamoja na kuwarudishia utukufu wao. Iko tayari kujitolea nafsi na kila chenye thamani kwake ili kulifanikisha jambo hilo.

---

[1]-Suuratul-Munafiqiin aya 8.
[2]-Suuratu-Aal-Imran aya 139.

Walhamdu Lillahi Rabbil-A`lamiin